Jumamosi Machi 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581603
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**ROONEY AFICHUA NIA YA KUWA KOCHA MAN UNITED**

UKURASA 22

**Mgogoro** ardhi wang'oa watano, kamati yaundwa

UKURASA 7



**Aliyefungwa** maisha jela kwa kubaka aachiwa huru

UKURASA 8

# Wosia wa Mwinyi kwa Watanzania




• **MAELFU** wamuaga Dar, Kikwete, Mpango wammwagia sifa, huzuni majonzi vyatanda Zanzibar... *Endelea Ukurasa 2,3&4*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa baba yake, Rais mstaafu Hayati Ali Hassan Mwinyi, kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. Nyuma ni mkewe, Mama Maryam Mwinyi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hali tete vifurushi NHIF, Ummy aita hospitali binafsi wayajenge

UKURASA 5



**MICHEZO** **SIMBA, JWANENG GALAXY MECHI YA MAAMUZI CAF** UK.24

**MAONI** UK.6

## BURIANI ALI HASSAN MWINYI





Jeneza lenye mwili wa Rais mstaafu Hayati Ali Hassan Mwinyi likiwasili kwa gari maalum la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wosia wa Mwinyi kwa Watanzania

**Na Restuta James**

RAIS wa Pili wa Tanzania, Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyefariki dunia juzi akiwa na umri wa miaka 98, ameacha wosia kwa Watanzania, ukiwa na angalizo dhidi ya ubaguzi wa kidini na kikabila, pia viongozi kutenda haki.

Wosia huo wa Mzee Rukhsa umo katika sura ya mwisho ya kitabu chake, 'Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu', unawataka Watanzania kuwa wavumilivu, kupenda haki na kuepuka ubaguzi wa kidini na kikabila.

"Ushauri wangu wa dhati kwa vizazi vya leo na vijavyo vya Watanzania ni kuwa tusije kulala usingizi. Ni rahisi sana kubomoa kuliko kujenga. Na kilichobomolewa kuja kujijenga upya ni kazi ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa wakati kinajengwa kwa mara ya kwanza.

"Kwa hiyo ndugu zangu Watanzania tusisinzie, wala kulala, kuhusu vita dhidi ya ukabila na udini narudia. Watanzania, viongozi na wananchi, msije katu mkafumbia macho mbegu zozote, hata ziwe ndogo kiasi gani, za ukabila na udini. Majuto ni Mjukuu," anaasa katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha yangu,' anasema.

Mzee Rukhsa pia anawataka Watanzania kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, katika vita hivyo.

"Mojawapo ya mambo ambayo Watanzania tunatakiwa daima kumuenzi nayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ni vita vyake vya dhati kabisa dhidi ya udini na ukabila.

Mwalimu alikuwa Mkristo kutoka bara tena bara yenyewe Mkoa wa Mara. Lakini akawa Dar es Salaam akawaunganisha Waislamu na Wakristo, watu wa bara na Pwani, kudai na hatimaye kufanikiwa kupata uhuru," anakumbusha.

Anasema uwezo na msimamo huo wa Mwalimu Nyerere, ulimpa nafasi ya kuchaguliwa kuongoza chama cha The Tanganyika African Association (TAA) na baadaye The Tanganyika African National Union (TANU) na kwamba waliofanikisha hilo ni wazee wa Kiislamu.

"Alilipa fadhila hiyo kwa kupiga vita udini na ukabila maisha yake yote ya uongozi wa siasa na serikalini," alisema.

Kwenye kitabu hicho, Mzee Mwinyi anaonya akikumbusha tahadhari iliyowahi kutolewa na Baba wa Taifa kwamba pamoja na sifa njema ya Watanzania kutobaguana kwa misingi ya kidini na kikabila, viongozi na wananchi wanapaswa kuupinga kwa kuwa wachache wenye tamaa ya madaraka wanaweza kuwagawa wananchi kwa msingi huo.

Anatoa mfano wa viongozi wa nchi za Afrika Mashariki wanavyopambana kuijenga jumuiya hiyo baada ya kuvunjika mwaka 1977. Kwa viongozi, Mzee Rukhsa anawataka wawe wavumilivu, wapende na watende haki.

"Pamoja na umuhimu wa uvumilivu, ni vyema viongozi wakawa wapenda na watenda haki kwa dhati, wanaojua na kuheshimu kwa vitendo haki za raia na kujali usawa wa binadamu.

"Kwa hulka yake, mwanadamu ana tamaa, ni mbinafsi. Hivyo akipata mwanya anaweza kupindisha Sheria kwa maslahi binafsi. Ni pale mahakama zitakapotekeleza majukumu yake vyema na kutetea haki na usawa wa kila upande, na kukwepa rushwa kabisa ndipo nchi itatawaliwa kwa haki na usawa na hivyo kutulia kisiasa na kiuchumi," anahitimisha Mzee Rukhsa wosia wake.

Akitangaza kifo cha Mzee Rukhsa juzi, Rais Samia alisema mwili wa kiongozi huyo utazikwa leo Mangapwani, Zanzibar.

## Maelfu ya wananchi wamuaga jijini Dar

**Na Christina Mwakangale**

MAMIA ya wakazi wa mkoa wa Dar es Salaam, wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wametia fora kwa kujitokeza na kujipanga kumuaga Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, wakati mwili wake ulipokatiza katika barabara kadhaa za mji huo.

Wanafunzi hao walijitokeza jana huku baadhi wakiimba nyimbo kama 'Tutaonana tenaaa,' 'Heshima umoja na amani', walishuhudiwa na Nipashe, kuanzia Mikocheni kupitia Morocco, Kinondoni hadi msikiti mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni na baadaye kwenda Uwanja wa Uhuru ambako ilifanyika hafla ya kuaga mwili wake.

Baada ya kutoka Kinondoni, msafara ulipita Mkwajuni na Magomeni Kanisani, Kigogo, Chang'ombe, Keko, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) hatimaye kuingia uwanjani hapo.

Umati wa wakazi wa mkoa huo, ulianza kujipanga barabarani mapema mkoani humo, huku maeneo kadhaa yakianza kushuhudia foleni, majira ya saa 5:00 asubuhi, ikiwamo eneo la barabara ya ITV, Mikocheni, ambayo ni miongoni mwa zinazokwenda nyumbani kwa Hayati Mwinyi.

Kadhalika, umati wa watu waliojipanga asubuhi walionekana kushangilia msafara wa magari uliobeba mwili wake, huku katika daraja la juu kituo cha Mwendokasi Morocco, baadhi wakikaa juu, ili kushuhudia msafara huo, uliokuwa unakwenda Uwanja wa Uhuru, mkoani hapa.

Kuanzia kona ya Kigogo, wakazi walifurika wakiwamo wanafunzi waliovalia sare za shule na msafara ulipofika eneo la Karume, ambako mara nyingi bidhaa huwa zimetandazwa chini na kuuzwa, kwa muda kadhaa biashara zilisitishwa na watu walisimama barabarani na kupunga mkono wa kwaheri.

MUDA MSAFARA

Mwili wa Hayati Mwinyi, ulianza msafara majira ya asubuhi kutoka nyumbani kwake Mikocheni mkoani Dar es Salaam, kwenda Msikiti wa BAKWATA, Kinondoni, kisha ukaanza msafara katika barabara kadhaa na uliwasili saa 8:00 mchana katika uwanja wa Uhuru, uliokuwa umejaa watu katika mzunguko wake, huku gwaride likianza jukumu la kiitifaki.

Katika uwanja huo, viongozi wa kitaifa walitangulia kufika kuusubiri mwili huo, wakiongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pamoja na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Dk. Abiy Ahmed.

Viongozi wakiwa wamesimama wima jukwaani pamoja na waombolezaji wengine, wimbo wa taifa ulianza kupigwa huku mwili ukiwa umezingirwa na kubebwa na maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wanane, wakitembea kwa mwendo wa pole.

Mwili wa Hayati Mwinyi, ulipelekwa katika eneo maalumu lililoandaliwa kwa ajili ya taratibu za kuaga. Baada ya kuwasili, Dakika chache baadae, sala ilianza, uwanjani hapo, ikiongozwa na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubery Bin Ally, kisha ratiba ya shughuli za mazishi ikaanza.

Swala hiyo ilipomalizika salamu za viongozi mbalimbali zilifuatia na baadaye kuaga mwili kisha safari ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ikafuata kupitia barabara za Nelson Mandela na Nyerere.

## BURIANI ALI HASSAN MWINYI



# Huzuni, majonzi vyatanda Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HUZUNI na majonzi vimetanda katika visiwa vya Zanzibar kutokana na kifo cha Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, huku wengi wakimwelezea kuwa alikuwa baba wa mabadiliko ya kiuchumi.

Akizungumza na Nipashe jana, mwanasiasa na mwanadiplomasia mkongwe, Balozi Amina Salum Ali, alisema Mzee Mwinyi alikuwa mwasisi mkubwa wa kuwainua wanawake katika nafasi za uongozi huku akibainisha kwamba katika baraza lake la mawaziri, aliwateua wanawake watano, akiwemo yeye.

Balozi Amina alisema Mwinyi alikuwa kiongozi shupavu na mzalendo ambaye atabaki kuwa baba wa mageuzi ya uchumi pamoja na siasa za mabadiliko kutoka chama kimoja kuingia mfumo wa vyama vingi.

Balozi Amina kwa mara ya kwanza aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mzee Mwinyi katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1985 na baadaye kuwa Waziri wa Nchi katika Wizara ya Mambo ya Nje.

Alisema Mzee Mwinyi atakumbukwa kwa kuwa ndiye aliyeleta mageuzi ya kisiasa kutoka katika mfumo wa chama kimoja hadi kuingia katika mfumo wa vyama vingi licha ya asilimia 80 ya Watanzania kutaka Tanzania ibaki katika mfumo wa vyama vingi.

"Mzee Mwinyi ni mtu aliyeniamini kunipa nafasi ya uongozi katika Wizara ya Fedha nikiwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo. Ni mtu ambaye akikupa kazi anakuamini na aliponipa nafasi aliniambia nakupa nafasi hii nina imani utaiweza," alisema Balozi Amina.

Pia alisema Rais mstaafu Mwinyi ndiye baba wa mageuzi ya kiuchumi ikiwamo kuyapokea mabadiliko makubwa ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) la kubadilisha uchumi wa Tanzania kutoka kumilikiwa na serikali na kushirikisha sekta binafsi na wananchi.

Mariyam Hamdani, aliyewahi kuwa Naibu Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) alisema katika kipindi cha uongozi wake ndiye aliyefanya juhudi za kuona sanaa na muziki wa taarab unarudi katika heshima yake pamoja na kuwatafuta wasanii wa kuimba nyimbo za Siti Binti Saada.

"Mzee Mwinyi alinitafuta mimi na Bi Kidude kuziibua nyimbo za gwiji mwimbaji na msanii wa Taarab za Siti Binti Saada na kuibua umaarufu wake wa zamani," alisema.

Pia alisema Mzee Mwinyi alikuwa muumini mzuri wa taarabu asilia lakini pia alisaidia kuikuza lugha ya Kiswahili.

Katibu wa Kamati ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, alisema taifa limepoteza kiongozi shupavu mwenye maono makubwa.

Alisema Mwinyi alikuwa kiongozi pekee aliyepata bahati ya kuhudumu kwa ngazi ya urais kwa upande wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na atakumbukwa kwa mageuzi na maendeleo makubwa ya kiuchumi kwa pande zote mbili za Muungano.

Pia alisema alipokuwa Rais wa Zanzibar, ndiye aliyeibua falsafa ya 'Zanzibar njema atakaye na aje' na kwamba yeye ndiye aliyefungua uchumi wa Zanzibar ikawa kimbilio la nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kati katika biashara.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Rais mstaafu Hayati Ali Hassan Mwinyi, kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikwete, Mpango wammwagia sifa Mwinyi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, amemwelezea Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi, kwa taswira tofauti huku akisema mbali na upole, alikuwa mwenye ujasiri, mvumilivu, mtu mwema na 'baba' wa mageuzi.

Akipanda jukwaani kutoa salamu za rambirambi katika hafla ya kuaga mwili wa kiongozi huyo aliyefariki dunia juzi, Kikwete alisema safari yake (Kikwete) ya kuwa Rais wa Tanzania, ilitengenezwa na Mzee Mwinyi, licha ya awali kuwa na matumaini zaidi katika jeshi.

Kikwete ni ofisa mwandamizi mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, aliyestaafu akiwa na cheo cha Luteni Kanali baada ya kuamua kubaki kwenye siasa mwaka 1992 kutokana na kuingia katika mfumo wa vyama vingi.

Alianza kumwelezea Mwinyi kama kiongozi aliyekuwa mvumilivu na asiyesita kufanya uamuzi akitolea mfano alipowaambia mawaziri wote wajiuzulu mwaka 1990, Kikwete akiwamo. "Rais Mwinyi ndiye aliyenianzishia safari ya kuwa Rais. Nilikuwa kwenye jeshi hamu yangu na matumaini ilikuwa huko na katika chama. Fundisho lingine kama kuna jambo unaliamini, komaa nalo. Alijiamini akavunja baraza la mawaziri mara mbili (safari nyingine ilikuwa mwaka 1994).

"Mimi nilimfahamu Mzee Mwinyi, wakati akiwa Waziri. Nilikuwa namsoma, namsikiliza katika taarifa ya habari, baadaye akajiuzulu, akawa Balozi, akarudi. Nilimfahamu kama mtu ambaye kwa kiingereza ni 'low profile'.

"Hakuwa mtu anayependa kujikweza, kimbelembele. Nilimfahamu vizuri zaidi mwaka 1984 wakati ule wa machafuko ya kisiasa Zanzibar. Kulikuwa na mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) nami nilikuwa mjumbe.

"Nikiwa nimeingia miaka miwili tu, tulipofika pale, wajumbe wote tukapangiwa kukaa kwenye hosteli za wanafunzi wa Chuo cha Biashara (CBE), si kawaida! Maana tulipewa posho wote na huwa tunatafuta sehemu za kulala.

"Baadae tulikuja kusimuliwa kwa nini lakini mawaziri na wale viongozi wengine walifikia kwingine ila tulikuwa na waziri mmoja tu aliyekuwa na sisi pale katika hosteli za CBE. Waziri huyo ni Ali Hassan Mwinyi, tukajiuliza kwa nini? Tukajifunza kwamba ile 'rest house' (nyumba ya kupumzikia Mawaziri) aliyopangiwa kukaa, waziri mwenzake aliamua kumweka mtu mwingine, akaondoka.

"Mzee Mwinyi alipofika pale (hosteli) alijua hiki ndicho chumba changu akaamua kuondoka na kuja kujiunga na sisi pale CBE. Alitupa mapenzi makubwa, hakuwa anadai kujaliwa tofauti na sisi wengine. Hakudai 'special treatment.' Tulikula wote, hapendi makuu," alisema.

Alisema anakumbuka pia wakati Mwinyi akipendekezwa jina lake kuwa Rais wa Zanzibar, alibaini Wazanzibar, wamepata kiongozi thabiti. Pia alisema kwa mara ya pili alimfahamu baada ya kumteua yeye kuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Kikwete alisema aliwahi kuwa waziri katika baraza lake la mawaziri kwa vipindi kadhaa, ikiwamo Waziri wa Fedha, katika uongozi wake na kwamba Mwinyi alikuwa msikivu, mpokea ushauri na mwenye kuamua bila woga.

"Unamuona ni mtu mpole, alililoamini kwa hili ni sawa, lina maslahi kwa taifa... Watanzania tumkumbuke kuwa baba wa mageuzi, mageuzi ya kiuchumi, mageuzi kisiasa.

"Mageuzi ya kisiasa iliundwa Tume ya Nyalali. Mapendekezo yalikuwa asilimia 80 tubaki na mfumo wa chama kimoja na 20 wanataka tuwe na mfumo wa vyama vingi. Aliamua jambo gumu tuwe na vyama vingi. Huo ndio uongozi," alisisitiza.

Pia alisema Hayati Mwinyi amemwachia mafundisho mengi, ikiwamo ujasiri huku hasa baada ya kuvunja baraza la mawaziri akivunja baraza la mawaziri mara mbili.

**MPANGO**

Akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya taifa, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alimwelezea Hayati Mwinyi kuwa alikuwa mtu mwema, mcha Mungu na mpenda dini tangu utotoni na mtu aliyesimama kidete kuitetea lugha ya Kiswahili.

Alisema Hayati Mwinyi anakumbukuwa kwa namna ya uongozi wake, kwa kuruhusu soko huria. Mpango, aliwaongoza waombolezaji waliofika uwanjani hapo, kwenye shughuli za mazishi na kuuaga mwili wa Hayati Mwinyi.

"Mungu alipenda kwamba azaliwe bara na alelewe Unguja. Amekuwa mzalendo. Kwa maneneo yake alisema maisha ya duniani ni hadithi, basi yafanye maisha yako hapa duniani kuwa hadithi, ameacha hadithi," alisema Dk. Mpango.

Baada ya Dk. Mpango kuaga mwili wa Hayati Mwinyi, alifuata mtoto wa marehemu, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe, Maryam, pamoja na wanafamilia.

**WARIOBA**

Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Joseph Warioba, alimwelezea Hayati Mwinyi kuwa kiongozi aliyeingia madarakani uchumi ukiwa katika mkwamo kutokana na vita, bidhaa zikiwa zinakwama kwa kukosa hata mafuta.

"Mzee Mwinyi alikuta kuna upungufu wa chakula. Aliunda timu ya kumsaidia kupambana na matatizo hayo, nikiwa mmojawapo. Tulifanya kazi usiku na mchana, baada ya miaka mitano, bidhaa zilikuwa zinapatikana kwa mikoa mitano baadaye.

"Mabadiliko makubwa alifanya lakini alisisitiza tusije tukaingia katika machafuko. Mzee Mwinyi ni mfano wa uongozi alikuwa kiongozi aliyepewa nchi ikiwa na mazingira magumu, akaweza. Tunaomboleza kwa kusheherekea maisha yake," alisema Warioba ambaye wakati wa ngwe ya kwanza ya urais wa Mwinyi alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

**MAOMBOLEZO**

Rais Samia Suluhu Hassan, alitangazia taifa kuwa katika maombolezo kwa siku saba kuanzia jana na kwamba maziko yatafanyika leo, Unguja. Pia alisema bendera zitapepea nusu mlingoti kwa siku saba kuanzia jana.

Hayati Mwinyi (98), amefariki dunia juzi katika hospitali ya Emilio Mzena, Kijitonyama, Dar es Salaam, akiugua maradhi ya saratani ya mapafu, akianza matibabu nchini Uingereza, tangu Novemba, mwaka jana.



# Simulizi visa na mikasa ya Mzee Mwinyi

**Na Restuta James**

JANA tuliangazia visa na mikasa ya Rais wa Awamu ya Pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ambaye kifo chake kilitangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan, juzi.

Visa na mikasa hiyo vilijumuisha kile anachokiita maajabu aliyoyaona kwa mara ya kwanza jijini London, Uingereza, mlango wa msalani ulipofunguka wenyewe baada ya kuwa ameukaribia. Ilikuwa mara yake ya kwanza kushuhudia maajabu hayo ya kiteknolojia.

Leo tunaendelea kuangazia visa na mikasa akiwa katika safari yake ya elimu ughaibuni.



Hayati Ali Hassan Mwinyi (kulia) wakiwa na mgeni wao, Walter Sisulu kutoka Afrika Kusini (wa tatu kulia), alipofanya ziara nchini mwezi Januari mwaka 1990. **PICHA: MAKTABA**

**MELINI KUREJEA ZANZIBAR**

Mwaka 1956 baada ya kumaliza masomo, Mwinyi, maarufu kama Mzee Rukhsa ambaye alizaliwa Mei 8, 2025, alikutana na vijana wenzake wawili (Dk. Awadhi na Makame), ambao walikuwa masomoni Uingereza, waliokuwa wanarejea nyumbani Zanzibar.

Wanafunzi kutoka nje ya Uingereza, walipewa uhuru wa kuchagua usafiri wa kuwarejesha kwenye nchi zao na walikuwa na hiari ya kupanda meli au ndege. Yeye na wenzie wakachagua kusafiri kwa meli ili kufanya utalii.

Katika kitabu chake Mzee Rukhsa: Safari ya Maisha Yangu, Mzee Mwinyi anasema ndani ya meli wao watatu walipewa chumba chao na ndicho kilichokuwa na watu weusi peke yao. Anasema muda mfupi kabla ya meli kung'oa nanga, waliletewa raia wa Somalia, akiwa amefungwa pingu na wakahisi atakuwa mhalifu mkubwa.

"Mimi na wenzangu tukashauriana kwa Kiswahili juu ya mbinu ya kusalimika tuwapo na bwana yule. Tukakubaliana tujenge urafiki naye. Tukawa tunachangishana fedha kidogo na kumkabidhi kwa ajili ya matumizi yake ikiwamo kumnunulia sigara," anasimulia.

Mzee Rukhsa anasema mhalifu huyo aliwasimulia matukio aliyofanya akiwa Uingereza yakiwamo wizi, unyang'anyi, kupigana na kubaka.

**KAHABA WA KIITALIANO**

Meli ya Doneta Castle waliyokuwa wanasafiria ilitia nanga bandari maarufu ya Genoa, Italia na Mzee Rukhsa, Dk. Awadhi na Makame, kama walivyokuwa abiria wengine, walishuka na kutembea ufukweni.

"Mara tukajiwa na dada mmoja wa Kiitaliano akamwendea na kumkumbatia Dk. Awadhi, kisha akamwita mwenziwe, 'Maria, Africano! Huyo Maria akaja na kwa pamoja wakatualika twende nao mahali ambapo walituambia wana vyumba tunakoweza kwenda kupumzika na kustarehe nao. Tukajua hawa ni makahaba na tukienda nao yanaweza kutukuta makubwa ikiwamo kuibiwa na hata kuuawa. Tukaamua kuwapa pesa kidogo waachane nasi, ikawa ndio mwisho wetu wa kupunga upepo," anasema.

**VITISHO VYA KABURU**

Hata hivyo, misukosuko wakiwa safarini haikuishia hapo kwa kuwa wakati meli inakatisha eneo la Suez Canal, majira ya mchana, joto lilikuwa kali na wakalazimika kwenda kupunga upepo kwenye sitaha ya meli.

Wakiwa wanapunga upepo wakati meli ikiendelea kukata mawimbi, alikuja kaburu mmoja wa Afrika Kusini na kueleza nia yake ya kutaka kupigana na Mwinyi na wenzie mmoja baada ya mwingine, kwa kile alichodai kuwa walimsukuma mke wake.

"Baada ya muda yule kaburu akarejea na kutuomba radhi, akasema mke wake amemwambia ametuonea bure, si kweli kwamba tulimsukuma... tukawa kimya tu.

Akaanza kukasirika tena, akidai kuwa si kawaida kwa yeye mzungu kuwataka radhi watu weusi na kwamba kama hatupokei maombi yake ya radhi basi ataondoka nayo, tukakubaliana tuipokee na kuachana naye, tukafanya hivyo, akaondoka."

Anasema mkasa huo uliibuka tena wakiwa dansi wakati wa jioni, baada ya kaburu huyo kuwafuata na kuwataka wacheze na mkewe mmoja baada ya mwingine hadi watakapochoka.

Kilichowaokoa Mzee Mwinyi na wenzie ni utulivu, kwani hawakukubaliana naye kwa kumwambia kwamba hawajui kucheza.

**ASAKWA NA POLISI**

Mwaka wa masomo 1961/62, alifadhiliwa na serikali kwenda kusoma katika Chuo Kikuu cha Hull, Leicester nchini Uingereza kwa ajili ya kujifunza mbinu za kufundisha ualimu kwa wanafunzi wa ualimu.

Siku moja, anasema alisahau mkoba wake mdogo uliokuwa na fedha katika duka moja alikokwenda kununua dawa ya meno mwishoni mwa juma. Kitendo hicho kiliwalazimu wafanyakazi wapige simu polisi ili imsake Mwinyi na kumrejesha dukani hapo kufuata mkoba wake.

Hata hivyo, kwa bahati nzuri, alifanikiwa kufika kabla hajatiwa mikononi mwa polisi kwa kosa la kupoteza fedha.

"Nikaenda (dukani), nilipofika karibu, mfanyakazi wa duka lile akaniwahi na kuniambia kwa sauti kubwa, 'umefuata pesa zako?' Akaifungua ile pochi akanihesabia pesa zilizokuwamo ndani yake akaniuliza je, ndizo pesa hizi, hazijapungua?."

"Baada ya wewe kuondoka hapa ndipo tukaiona hii pochi hapa mezani. Tukajua ni yako. Hivyo tulipiga simu polisi na kuwapa wasifu wako ili ukamatwe na kurudishwa hapa tukukabidhi pesa zako," anasema.

**UTEUZI UWAZIRI**

Miaka miwili baada ya Mzee Rukhsa kurejea Zanzibar, yalitokea Mapinduzi matukufu yaliyoung'oa utawala wa Sultan na kuanzisha utawala wa wananchi walio huru; hatua ambayo pamoja na mambo mengine iliacha ombwe la nafasi za uongozi ndani ya utumishi wa umma.

Serikali ya wananchi huru ikateua wananchi waliokuwa na elimu kushika nyadhifa za utumishi na Mwinyi akateuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, akitokea Chama cha Walima Karafuu (CGA).

Baadaye serikali za Zanzibar na Tanganyika, zilikubaliana kuungana na kutoa fursa kwa wananchi wa pande zote kufurahia matunda ya umoja huo na Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliteua mawaziri kadhaa kutoka visiwani.

"Siku moja Desemba 1970, wakati nakaribia kutoka kazini hapo CGA, nikapokea simu kutoka Ikulu, Zanzibar, nikiambiwa naitwa na Rais Abeid Amani Karume.

Fikra za kila aina zikanijaa kichwani. Sikujua naitiwa nini na kama nitakuwa salama," anasimulia na kubainisha kuwa dakika chache mbele, alifuatwa na gari la polisi ili impeleke Ikulu.

"Nikakataa kuipanda, nikawaambia walionifuata na hilo gari kuwa kwa vile mimi si mfungwa au hata mtuhumiwa, sioni kwa nini wanibebe na gari lao. Nikawaambia nitakuja mwenyewe. Nikaingia kwenye gari langu dogo aina ya Morris Minor nikaanza kujiendesha mwenyewe kuelekea Ikulu na wao wakinifuata nyuma na gari lao huku wakiwasha taa na kupiga honi."

Anasema alilikuta geti la Ikulu likiwa wazi kwa kuwa walinzi walimtegemea. Alianza kupanda ngazi kuelekea ofisini kwa Hayati Karume akiwa mwenye hofu nyingi.

"Nikamwona kwa mbali amekaa kimya, katulia kama mwenye fikra nyingi. Sikumshtua na nikajipa muda na mimi nitulie, nijifute jasho na kukusanya pumzi," anasema.

Alipojiridhisha kwamba ametulia, anasema ndipo alipomwamkia Rais Karume ambaye alimkaribisha na kumweleza lengo la kumwita na kwa kuwa alikuwa amependekeza jina lake kwa Rais Julius Nyerere ambaye alikuwa anaunda Baraza la Mawaziri.

Taarifa hiyo kutoka kwa Hayati Karume, anasema aliifurahia na kulazimika kufuatilia taarifa ya habari saa 2:00 usiku na siku hiyo aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

## CCM, CHADEMA waeleza atakavyokumbukwa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), vimemwelezea Hayati Ali Hassan Mwinyi kwamba atakumbukwa kwa mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii aliyoyafanya wakati wa uongozi wake.

Taarifa kwa vyombo vya habari zilizotolewa na vyama hivyo pia zilieleza kuwa Hayati Mwinyi atakumbukwa alivyosimamia mageuzi ya sera za kiuchumi na kuruhusu mifumo ya uhuru wa soko, sera.

Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema Mzee Mwinyi atakumbukwa kwa mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii aliyoyaongoza wakati akiwa Rais wa Tanzania. Mwinyi alikuwa Rais wa Tanzania mwaka 1985 hadi 1995.

"Jitihada zake kubwa katika kuleta mabadiliko ya kiutendaji, kiuendeshaji na kimfumo ndani ya chama chetu alipokuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa kuanzia mwaka 1990 hadi 1996 zitakumbukwa,". alisema Dk. Nchimbi.

Balozi Nchimbi alisema mchango wake utakumbukwa kwa namna alivyosaidia kujenga umoja wa kitaifa na kulinda muungano, mojawapo ya tunu za taifa wakati wa utumishi wake serikalini.

"CCM itaendelea kumuenzi Mzee Ali Hassan Mwinyi kwa yale yote mema aliyotuusia na kututendea. Tunamwombea apumzike kwa amani na tunawaombea familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema watamkumbuka Hayati Mwinyi alivyosimamia mageuzi ya sera za kiuchumi za Tanzania na kuruhusu mifumo ya uhuru wa soko, sera ambayo imekuwa ndio msimamo wa chama chao katika kukuza uchumi na kuchochea maendeleo.

"CHADEMA kimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Hayati Mzee Mwinyi tunaungana na Watanzania kuomboleza msiba huu wa kitaifa," alisema Salum.

Alisema wanatoa pole kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wajane wa marehemu, familia, ndugu, jamaa na marafiki.

"Kama alivyowahi kusema wakati wa uhai wake kuwa maisha ni hadithi naye ameikamilisha hadithi ya maisha yake, atakumbukwa kwa hekima, busara uwajibikaji na kujituma kwake wakati wote akiwa Rais na hata kabla aliposhikilia wadhifa wa Rais wa Zanzibar, nafasi nyingine mbalimbali serikalini ikiwamo nafasi ya uwaziri na ubalozi wa Tanzania nchini Misri," alisema.

Alisema Mwenyeti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ataongoza ujumbe wa chama katika maziko yaliyopangwa kufanyika leo mjini Unguja.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alitaja mambo manne ya kumuenzi Hayati Mzee Mwinyi ikiwamo kukamilisha kwa mageuzi ya kiuchumi.

"Wakati anakuwa Rais nchi ilikuwa katika hali ngumu ya kiuchumi akahitimisha majadiliano na nchi hisani na mashirika ya kimataifa na kuunda timu iliyotoa mapendekezo ya mageuzi ya uchumi," alisema Mnyika.

# Hali tete matibabu NHIF, Waziri awaita hospitali binafsi wayajenge

**Na Waandishi Wetu**


Ummy Mwalimu

HALI ya matibabu jana ilikuwa tata katika baadhi ya hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya nchini, baada ya kuanza kutumika kwa vitita vipya vya matibabu vilivyotangazwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Wakati hali ikiwa hivyo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amewataka wamiliki wa hospitali binafsi kurejea kwenye meza ya mazungumzo ili kuangalia kero na kuzitatua.

Jana ilikuwa siku rasmi ya kuanza kutumika kwa vitita vipya, lakini baadhi ya hospitali binafsi ziligoma kuwapokea wagonjwa wanachama wa NHIF na kuwaelekeza kwenda katika hospitali za serikali, huku baadhi zikikubali kuwahudumia.

Nipashe lilipita katika baadhi ya hospitali nchini na kuona huduma zikitolewa katika baadhi ya hospitali huku zingine zikisitisha huduma.

Katika Jiji la Dodoma, Nipashe ilitembelea hospitali binafsi za Agakhan, JMS na Mwangaza na kubaini baadhi zimeendelea kupokea wagonjwa wa NHIF, huku zingine zikisitisha kuwahudumia. Hospitali ambazo zimeendelea kupokea wagonjwa wenye kadi za NHIF ni JMS na Mwangaza, huku Agakhan ikiwarudisha wagonjwa wenye kadi hizo, hivyo kukosa matibabu. Katika Hospitali ya Agakhan, wagonjwa waliofika eneo la mapokezi, walipewa majibu kwamba hawawapokei.

Mmoja wa wagonjwa ambaye alikumbana na hali hiyo, Zainabu Hussein, alisema amefika hospitalini hapo akiwa na miadi na daktari kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa ujauzito wake, lakini alipewa jibu kwamba hawapokei wenye kadi za NHIF.

"Leo nimekuja hapa kwa ajili ya kupata vipimo kwa daktari wangu, lakini nashangaa natoa kadi yangu ya bima naambiwa kuwa leo hawapokei bima na mimi sina hela inanilazimu nitoke hapa niende kutafuta hela kwa ajili ya vipimo"alisema.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Pendo Meshack, alisema ameacha vipindi ili kupata vipimo katika hospitali hiyo lakini amekutana na mgomo huo ambao umesababisha kukosa matibabu.

**ANDA YA KASKAZINI**

Katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Nipashe lilifika katika baadhi ya hospitali na vituo binafsi vya kutolea huduma za afya Kilimanjaro na Arusha na kukuta vinaendelea kutoa huduma na kuwapokea wagonjwa wenye kadi za NHIF.

Mkoani Kilimanjaro, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Hospitali Teule ya St. Joseph na Hospitali Teule ya Machame, huduma za NHIF zilikuwa zikiendelea kutolewa.

Katika mkoa wa Arusha, Hospitali ya Seliani LMC na St. Joseph nazo zilikuwa zikiendelea kupokea wagonjwa wenye kadi za NHIF.

Mmoja wa watoa huduma ambaye hakutaka jina lake kuandikwa, alisema: "Sisi tutaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotumia bima ya afya hadi pale Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu atakapo toa tamko."

**MWANZA SHIDA**

Katika Mkoa wa Mwanza baadhi ya wagonjwa wanaotibiwa na NHIF walieleza kutokupata huduma katika baadhi ya hospitali binafsi, huku wakitakiwa kulipia kawaida ili kuhudumiwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa mashariti ya kutokutajwa majina, wagonjwa waliofika katika Hospitali ya Mwananchi iliyoko jijini Mwanza, walisema baada ya kufika hospitalini hapo waliulizwa kama wanatumia NHIF na walipokubali waliambiwa kwa sasa huduma hiyo haitolewi.

Ilipofika majira ya saa 10:25 jioni mwandishi wa Nipashe alifika hospitalini hapo akiwa na kadi ya NHIF, lakini mmoja wa wahudumu alimwambia kuwa hawezi kupewa huduma.

Mwandishi wa Nipashe alitembelea hospitali binafsi ya Royal, jijini Mwanza na kufanya mahojiano na mmoja wa madaktari ambaye hakutaka jina lake kutajwa. Daktari huyo alisema wamesitisha kupokea wagonjwa wanaotumia kadi za NHIF mpaka pale watakapoweka utaratibu mwingine.

**MSIMAMO DAR**

Katika Jiji la Dar es Salaam hospitali saba za binafsi zilisimamia kile kilichoelezwa kuwa zitasitisha huduma hiyo. Hospitali hizo ni Regency, Medical Center, TMJ, Kairuki, Apolo na Aga Khan.

Katika Hospitali ya TMJ kuliwekwa tangazo liloeleza: "Uongozi wa kituo unapenda kuwafahamisha wanachama wa NHIF kwamba kuanzia Machi 1, 2024 saa 6:01 usiku hatutatoa huduma kwao mpaka utaratibu maalum wa kuwapokea utakapojulikana.

"Tunawashauri wanachama hao wapige simu NHIF ili kujua namna wanatavyoendelea kupata huduma"

Katika Hospitali ya Regency, tangazo kama hilo lilibandikwa katika maeneo kadhaa na kuongeza kuwa: "Tunawashauri wanachama wapige simu NHIF ili kujua namna watakavyoendelea kupata huduma."

Katika Hospitali ya Kairuki, tangazo lilisema: "Uongozi wa Kairuki unapenda kuwafahamisha wanachama wa NHIF kwamba kuanzia Machi 1, 2024 saa 6:01 usiku hatutatoa huduma kwao mpaka utaratibu maalum wa kuwapokea utakapojulikana.

"Tunawashauri wanachama hao wapige simu NHIF ili kujua namna watakavyoendelea kupata huduma. Aidha wateja wetu wanaweza kuendelea kupatiwa huduma kwa kutumia bima zingine zinazopokelewa Kairuki Hospitali au kulipa pesa taslim"

Mmoja wa wagonjwa aliyekutwa na Nipashe katika Hospitali ya Regency, Collin Lema, ambaye alimpeleka mzazi wake kusafisha damu, alisema alikutana na usumbufu katika kutumia bima ya NHIF hali iliyowalazimu kulipia Sh. 250,000 ili kupatiwa huduma hiyo.

**MBEYA**

Nipashe lilifika katika Hospitali ya Maranatha, jijini Mbeya na kushuhudia wananchi wakiendelea kuhudumiwa kwa kutumia NHIF licha ya msimamo wa Chama cha Wenye Hospitali Binafsi (APHFTA) wa kusitisha huduma kwa wateja wanaohudumiwa na bima hiyo.

Baadhi ya wananchi ambao walikutwa wakipata huduma kwenye hospitali hiyo walisema walihudumiwa kama ilivyokuwa awali na hawakukumbana na usumbufu wa aina yoyote.

**WAZIRI AWAITA MEZANI**

Waziri Ummy jana katika taarifa yake kuhusu msimamo wa serikali, aliwaagiza watoa huduma hao kuendelea kutoa huduma na endapo kuna shida katika kitita hicho, warudi katika meza ya majadiliano na serikali badala ya kusitisha huduma.

Ummy alisema gharama za mwisho ambazo zimewekwa katika kitita Januari 4, mwaka huu, alikutana na timu yake ya wataalamu wa wizara ambao walifanya kikao cha pamoja na wadau wa NHIF.

Alisema katika kikao hicho walikuwepo wamiliki wa vituo vya afya binafsi, Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC), Kamati ya Afya chini ya Bakwata, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Chama Cha Madaktari Tanzania (MAT) na NHIF kwa lengo la kusikiliza hoja za wadau.

Januari 4, mwaka huu, alisema wizara iliamua kusitisha utekelezaji wa kitita kipya cha NHIF cha mwaka 2023 na kuunda kamati yenye wadau kutoka serikalini, sekta binafsi na taasisi za bima kwa ajili ya kuishauri serikali.

"Kwa sababu hakuna vigezo vingine waje mezani watueleze tumewawekea faida ndogo kwa kutueleza dawa wamenunua kwa kiasi gani? na gharama za uendeshaji zipoje? waje waseme kama dawa hii haiuzwi bei fulani sio mseme hatutaki kitita. Leteni hoja zenu mezani. Kamati naipongeza imefanya kazi nzuri," alisema Waziri.

Alisema kamati hiyo imeweka gharama za uchakavu wa vifaa vinavyotumika.

"Nawaomba warudi kwenye meza ya mazungumzo. Kamati imeweka vigezo, waje waseme vigezo hivi havipaswi kutumika katika kutoa huduma za afya," alisema.

Waziri alisema baada ya kupata taarifa ya kamati aliitisha kikao kingine Februari 17 na kuwapatia taarifa hiyo, hakuna hata mmoja aliyesema hawakubaliani na vigezo hivyo.

Waziri Ummy alisema NHIF kuna vitu ambavyo wamepoteza na wao wanatakiwa wakubali baadhi ya vitu kupoteza.

"Tumewaelekeza NHIF kuendelea kupokea maoni ya wadau kuhusiana na kitita hicho wakati wa utekelezaji. Naomba nieleze kumekuwa na ushirikishwaji mkubwa wa wadau katika mchakato huo nimewasikiliza mimi na timu yangu tangu mwaka 2022 tunachelewa lakini tumekuwa wavumilivu milango ya wizara ipo wazi," alisema huku akisisitiza kwamba mtoa huduma kwa mwanachama wa NHIF anatakiwa kutambua ameingia mkataba na NHIF wa kutoa huduma.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale, Beatrice Shayo (Dar) na Paul Mabeja, (Dodoma), Woinde Shiza (Arusha) Mary Mosha (Moshi), Nebart Msokwa (Mbeya), Zatifa Ramadhan, Rose Jacob, Vitus Audax (Mwanza).**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanamichezo, wasanii tuyaenzi mema ya Rais Ali Hassan Mwinyi

**JUZI** Taifa la Tanzania lilipata pigo lingine baada ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi.

Kifo cha Rais huyo maarufu kwa jina la Mzee Rukhsa kilitangazwa juzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ikiwa ni siku chache baada ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Ngoyai Lowassa.

Rais Mwinyi, ambaye aliliongoza Taifa la Tanzania kuanzia mwaka 1985 mpaka mwaka 1995 akipokea kijiti kutoka kwa Rais wa kwanza na mwasisi wa taifa letu, Julius Nyerere.

Kifo cha Rais Mwinyi kimewashtua watanzania wengi lakini kimekuwa pigo kwa taifa kwa kuondokewa na mmoja wa wazee wa taifa hili, lakini pia nyanja ya michezo na burudani imeondokewa na mtu muhimu aliyesaidia mambo mengi katika kukuza michezo na sanaa kwa ujumla.

Wengi tunaufahamu na kuukumbuka msemo maarufu wa ' kichwa cha mwendawazimu', huu ni msemo ambao Rais Mwinyi aliutoa mwaka 1993 baada ya matokeo mabaya ya klabu za Tanzania na timu ya taifa kwenye mashindano mbalimbali akifananisha na kichwa cha mtu ambacho kila kinyozi anakuja kujifunzia hapo kunyoa.

Kauli hii ilikuwa maarufu ikielezea unyonge wetu kwenye mashindano mbalimbali, hata hivyo baada ya vilabu vyetu na timu ya taifa kuanza kufanya vizuri, Rais Mwinyi akiwa tayari kashatoka madarakani alifuta kauli hiyo.

Rais Mwinyi atakumbukwa kwa mambo mengi sana na wanamichezo na wasanii katika kukuza na kuendeleza sekta hizo.

Rais huyo wa awamu ya pili enzi ya uhai wake na hasa alipokuwa madarakani alikuwa na kiu ya kutaka kuona michezo nchini inakuwa na kuitangaza nchi kimataifa.

Haikushangaza mwaka 1993 wakati Simba ilipoingia hatua ya fainali ya kombe la CAF (sasa Kombe la Shirikisho Afrika), Rais Mwinyi alikubali kuwa mgeni rasmi kwenye mechi ya marudiano ya fainali ya michuano hiyo dhidi ya Stella Abidjan ya Ivory Coast.

Mzee Rukhsa ndiye aliyewavalisha medali mabingwa wa michuano hiyo, Stella Abidjan pamoja na washindi wa pili, Simba.

Ikumbukwe kuelekea mchezo huo wa fainali, aliyekuwa mdhamini wa Simba wakati huo, Azim Dewji, alitoa ahadi ya kuwapa wachezaji wa Simba magari aina ya Kia kama watatwaa kombe hilo, lakini walishindwa kulichukua na mdhamini kuacha kununua.

Hata hivyo baadae alikubali kuwanunulia wachezaji wa Simba magari madogo aina ya Toyota Corolla na Rais Mwinyi kwa kutambua jitihada za wachezaji wa Simba, aliamuru kuondoa ushuru kwa magari hayo ili wachezaji wayapate bila kikwazo.

Wakati wa utawala wake, mwaka 1994, Tanzania Bara ilifanikiwa kutwaa kombe la Challenge lililofanyika nchini Uganda.

Mbali na hilo, Simba walipotinga kwa mara ya kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuwaondoa waliokuwa mabingwa watetezi, Zamalek mwaka 2003, Rais Mwinyi aliongoza mapokezi ya timu hiyo kutokea Misri

Kwa kuonyesha kupenda michezo, Rais Mwinyi akiwa nje ya madaraka ya uraisi, alikubali kuwa mlezi wa Shirikisho la Ngumi za Ridhaa Tanzania (BFT) chini ya Mwenyekiti wake Alhaji Sahaban Mintanga.

Haya yote aliyafanya akiwa na lengo la kuona michezo Tanzania inakuwa na kusonga mbele, ni vyema wanamichezo kuenzi yale mambo mazuri aliyoyafanya Rais Mwinyi kwenye michezo.

Tunaamini kuondoka kwake kutawapa chachu wanamichezo kuhakikisha wanayaenzi na kuyaendeleza mambo mazuri aliyoyafanya Rais Mwinyi kwenye michezo.

Daima jamii ya wanamichezo itamkumbuka Rais Mwinyi, tunaungana na watanzania wengine kuwapa pole familia ndugu na jamaa na kumuombea Mzee Rukhsa apumzike kwa amani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwinyi alivyosaidia wachezaji Simba kuzawadiwa magari

**RAIS** wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, aliyefariki dunia juzi akiwa na miaka 98 atakumbukwa kwa mengi katika nyanja mbalimbali, huku mashabiki wa michezo wakimkumbuka kwa kukuza na kuendeleza sanaa na michezo nchini.

Wakati wa utawala wake ndicho kipindi ambacho klabu ya Simba ilifanikiwa kutinga fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) mwaka 1993 na kufungwa mechi ya fainali mabao 2-0 dhidi ya Stella Abidjan ya Ivory Coast, mechi iliyochezwa Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Novemba 27, 1993, na yeye kuwa mgeni rasmi.

**Mwinyi ndiye aliyewavisha wachezaji wa timu zote mbili medali, Simba wakivalishwa medali ya fedha na mabingwa wakipata ya dhahabu.**

Mwinyi ndiye aliyewavisha wachezaji wa timu zote mbili medali, Simba wakivalishwa medali ya fedha na mabingwa wakipata ya dhahabu.

Katika mechi ya kwanza, Simba ilitoka suluhu ugenini, lakini kwa namna ya kushangaza ilipoteza nyumbani mbele ya Rais Mwinyi wakati huo.

Awali Simba iliahidiwa kupata magari aina ya Kia kila mmoja wakati huo kutoka kwa mfadhili wao wakati huo, Azim Dewji, lakini ahadi ilikuwa imekufa baada ya kufungwa, lakini chini ya utawala wake, akaona haikuwa vyema wachezaji wa timu hiyo kutopata chochote kwani walifanya kazi kubwa hadi kufikia hatua hiyo.

Ndipo kwa kushirikiana na mfadhili huyo, wakaamua kuagiza na kuwazawadia wachezaji 30 wa Simba magari aina ya Toyota Corolla, wakati huo magari hayo yalikuwa kisasa kabisa.

Serikali ya Mwinyi iliondoa kodi ili kupunguza gharama nyingi zilizokuwa zikihitajika, na kwa kiasi kikubwa yaliwasaidia sana baadhi ya wachezaji waliokuwa wanastaafu mwaka huo kujikimu kimaisha kwa kuyageuza kuwa taxi.

Kutokana na kipigo hicho, na baada ya hapo kukawa na mfululizo wa matokeo mabaya ya timu ya taifa yaliyomchukiza Rais Mwinyi na kufikia kusema soka la Tanzania ni kama kichwa cha mwendawazimu kiasi kwamba hata mlevi anajifunzia kunyoa.

Msemo huo aliufuta miaka mingi baadaye, na hiyo ni baada ya kuona mambo yanabadilika na angalau klabu za Tanzania zinafanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa na timu ya taifa 'Taifa Stars' pia ikionekana kuamka.

Mwaka mmoja baadaye, 1994 chini ya utawala wake, Tanzania Bara ilifanikiwa kutwaa Kombe la Challenge nchini Uganda.

Kwa upande wa muziki, kipindi cha Mwinyi ndicho bendi nyingi zilianzishwa ukiacha zile kongwe na hii ilitokana na urahisi wa upatikanaji wa vyombo vya muziki ambavyo awali ilikuwa ngumu kuvipata na kusababisha bendi nyingi kufa.

Rukhsa ya mzee Mwinyi, mbali na vitu vingine kuruhusiwa kuingia nchini, pia vyombo vya muziki viliruhisiwa kwa wingi kiasi cha bendi nyingi kuanzishwa na kuleta upinzani na ushindani mkali, muziki wa Tanzania ukazidi kuja juu.

Pia Hayati Mwinyi alikuwa mwanamichezo, yeye mwenyewe alisema alipokuwa kijana alikuwa akicheza beki wa kati, na moja kati ya vitu vilivyomfanya aishi miaka mingi ni mazoezi ya kukimbia, maarufu kama 'Jogging'.

Alikuwa akiwashinda hata wale wenye umri mdogo ambao walikuwa wakiishia kati na yeye kumaliza mzunguko wote wa mbio zilizopangwa.

Hivi ndivyo wasanii, wanamuziki na wanamichezo wanavyomkumbuka Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, Mzee Rukhsa.

## HABARI KITAIFA

# Wanawake ni injini ya maendeleo na ustawi

**Na Dk. Mohamed Maguo**

TANZANIA imejaliwa na kubarikiwa kuwa na wanawake jasiri, shupavu na shujaa wenye mchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha ustawi wa jamii na kuiletea nchi yetu maendeleo.

Aidha, imeelezwa kuwa wanawake ni watu wasiokata tamaa katika maisha hali ambayo imewawezesha kufikia ngazi za juu katika elimu na maisha kwa jumla.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) anayesimamia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Deus Ngaruko, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wasichana wa foundation mkondo wa sayansi kwenye ukumbi wa OUT mkoani Singida.

"OUT ina imani kubwa sana na uwezo wa wasichana katika kufanya vizuri kwenye masomo yao. Ninyi ni wasichana ambao hamkufanya vizuri katika masomo ya sayansi sekondari na diploma kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukatili wa kijinsia, umasikini, ujauzito na wazazi kutengana.

"Sasa mmepata fursa hii ya kusoma programu ya foundation na mkimaliza mtajiunga ngazi ya shahada ya kwanza. Tunawaamini kwamba mnaweza kwa sababu wasichana ni mabingwa wa kutokata tamaa katika maisha. Tumieni muda wenu vizuri katika masomo ili asiwepo hata mmoja ambaye atashindwa kufaulu hii foundation," alisema.

"Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia mradi wa Mageuzi ya Elimu ya Juu kwa Maendeleo ya Kiuchumi (HEET) imewapatia ufadhili wa asilimia 100, hivyo jukumu lenu ni kusoma kwa bidii ili mfaulu mwedelee ngazi ya shahada ya kwanza," alisisitiza.

Prof. Ngaruko alisema jamii ya Watanzania imelelewa na wanawake na kufika katika ngazi za juu za elimu na kufanikiwa katika maisha, akitolea mfano wake.

"Mimi binafsi nililelewa na dada yangu ambapo tulikuwa wadogo zake wanne. Mara tu baada ya baba yetu kufariki dunia, mimi nilikuwa na umri wa miaka mitano na wakati huo dada yetu alikuwa amemaliza kidato cha Nne na kufaulu kwa daraja la kwanza.

Pamoja na ufaulu huo mkubwa, hakwenda kidato cha tano badala yake akajiunga na programu maalumu ya ualimu akawa mwalimu. Lengo lake lilikuwa ni ili aweze kupata kazi ambayo itamwezesha kutulea sisi wadogo zake. Alitulea vizuri na baadae akaolewa na kupata watoto na familia inayomtegemea ikawa kubwa lakini bado aliweza kuimudu," alisema.

Alisema baadae alijiendeleza kwa kufanya mtihani wa 'mature age entry wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kufaulu kisha kuendelea na masomo ya Shahada ya kwanza kufaulu daraja la kwanza, akabakishwa kuwa mhadhiri.

Baada ya muda mfupi, alisoma mpaka shahada ya uzamivu na kuwa profesa mapema kabisa na kuwapita hata wanaume ambao aliwakuta kama wahadhiri na yeye akiwa mwanafunzi.

# Migogoro ardhi yang'oa watumishi watano

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewasimamisha kazi watumishi watano wa idara ya ardhi katika Manispaa ya Kahama kutokana na kuwa sehemu ya migogoro ya ardhi kwa wananchi.

Waliosimamishwa kazi ni pamoja na Mkuu wa Idara ya Ardhi, Clemence Mkusa, Ofisa Ardhi Mteule, Yusufu Shabani, Mpima Ardhi, Yahya Msangi, pamoja na Ofisa Mipango Miji, Crispina Kisengo na hatua hiyo imechukuliwa hadi uchunguzi utakapofanyika.

Mndeme alifikia uamuzi huo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Majengo, akisikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi husasani sekta za elimu, afya, ardhi pamoja na miundombinu ya barabara.

Alitaja makosa yanayowakabili watumishi hao ni utovu wa nidhamu, kupima na kutoa hati miliki kwenye viwanja vyenye hati miliki kwa watu zaidi ya watano na kusababisha migogoro ya muda mrefu ambayo imekuchukua muda kutafutiwa ufumbuzi, huku wajane wakiongoza kukosa haki zao.

Mkuu wa mkoa alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Prof. Sisa Tumbo, kuunda kamati ya kuwachunguza na itakapobaini makosa haya, wachukuliwe hatua stahiki ikiwamo kufukuzwa kazi.

"Haiwezekani kila mwananchi anayesimama kutoa malalamiko au kero yake ni ardhi na kuwataja watu hawa kuwa chanzo cha kuwepo kwa migogoro, hivyo ninawasimamisha kazi kupisha uchunguzi," alisema.

Prof. Tumbo aliahidi kuunda kamati itakayochunguza tuhuma hizo na kuwasilisha kwa wakati, watakaobaina kuhusika watawaondoka kazini moja kwa moja.

Mmoja wa wananchi waliwasilisha malalamiko ya kupokwa ardhi kwa madai inarejeshwa serikali, Caroline Magege, alisema eneo lake limepimwa na kutoka viwanja 19, kati ya hivyo viwanja vitano ameshapata hati miliki na viwanja 14 wamemilikishwa watu wengine.

Alisema anachotaka ni kurejeshewa maeneo yake kwa kuwa yako ndani ya uzio wa nyumba anayoishi na hivi karibu mgambo wa manispaa walifika na kubomoa uzio wake ili wenye hati miliki wavijenge na kuomba serikali kuingilia kati na kuvirejesha kwake.

Mkazi mwingine, Maimuna Misana, alisema ana eneo Mtaa wa Mwanva ambalo limepimwa na kutoa viwanja 30, kati ya hivyo 29 amemilikishwa isipokuwa kimoja kimechukuliwa kwa madai ya kupewa Jeshi la Polisi.



Mbunge wa Moshi mjini, Priscus Tarimo (katikati), akizungumza na viongozi wa waendesha bodaboda na bajaji wa Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro hivi karibuni, kabla ya kuwagawia vizibao viakisi mwanga (Reflector) kwa bodaboda zaidi ya 800 kwa lengo la kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa weledi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Hongo ya sh. milioni 8 yampeleka jela

**Na Joctan Ngelly,** KAGERA

MAHAKAMA ya Wilaya Missenyi Mkoa wa Kagera imemhukumu Rehema Mdaki (46) mkazi wa Shinyanga kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Sh. milioni moja kwa kosa kutoa rushwa ya Sh. milioni nane.

Alitoa fedha hizi kwa ajili ya kukomboa mzigo wa dawa za kilimo wenye thamani ya Sh. milioni 30 uliokamatwa kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda, kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Yohana Myombo, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kasa pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Myombo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kutoa hongo kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera, Kelvin Murusuri, ambaye alipeleka mahakamani mashahidi sita na na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Hakimu Myombo alisema siku ya tukio, Agosti 29, 2023 katika Wilaya ya Missenyi mshtakiwa alikamatwa na fedha za hongo Sh. milioni nane alizokuwa anapeleka kuhonga kwa ajili ya kukomboa mzigo wake uliokuwa umekamatwa Mei 30, 2023 katika mpaka wa Mutukula.

Alisema fedha hizo zilikuwa zimekusudiwa kuhongwa maofisa wa serikali wa mpaka wa Mutukula ambao ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kilimo na Mionzi, kabla hawajapewa hizo fedha, TAKUKURU walipata taarifa na kuingilia mawasiliano kisha kuweka mtego na kumkamata mshtakiwa akitoa hongo kupitia ofisa aliyependikizwa kupokea hizo fedha. Hakimu Myombo alisema amesikiliza pande zote na kubaini kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasina kuacha shaka yote na mshtakiwa mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa uliloshtakiwa nalo. Pia mahakama hii inakutaka utowe maombolezo ili iweze kukupunguzia adhabu.

Upande wa mashtaka, ukiongozwa na Wakili Murusuri, uliomba mahakama itoe adhabu kali iwe fundisho kwa wafanya biashara ambao wanawahonga watumishi wa umma kwa kutaka kupata nafuu na kukwepa mapato ya serikali.

Aidha, Wakili Murusuri aliomba mahakama itaipishe fedha za hongo zilizokamatwa na kuwa mali ya umma.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Geofrey Binamungu ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa aliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa sababu ana familia inamtegemea.

Hakimu Myombo alisema amezingatia maombi ya pande zote mbili na kumhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh milioni moja kuwa fundisho kwa wafanyabiashara wanaokwepa kulipa mapato ya serikali na ameridhia maombi ya kutaka fedha zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

# Aliyefungwa maisha kubaka aachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania kanda ya Iringa, imemwachia huru Method Mhimba aliyefungwa maisha jela kwa kubaka baada ya kubaini alitiwa hatiani kimakosa na kiwango cha upelelezi katika shauri hilo kilikuwa duni.

Mahakama hiyo mbele ya Jaji Eliamani Laltaika, ilimwachia huru Mhimba jana baada kukubali rufani yake ilivyokuwa na hoja tano za kupinga hatia na adhabu aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Iringa.

Ilidaiwa kati ya mwaka 2018 na 2021 maeneo ya Mlandege, Manispaa ya Iringa, mrufani alimnajisi binti wa miaka 10.

Katika shauri hilo, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watatu akiwamo binti, daktari na mama wa mwathirika wakati upande wa utetezi wa mrufani ukiwa na mashahidi wawili ambao ni yeye na mkewe.

Baada ya usikilizwaji wa shauri, Mahakama ya Wilaya ya Iringa ilimtia hatiani mrufani na kumhukumu kifungo cha maisha jela na kuamuru alipe fidia ya Sh. milioni tano.

Mhimba alipinga adhabu hiyo kwa kuwasilisha sababu tano, ikiwamo mahakama kukosea kumtia hatiani wakati upande wa mashtaka haukuthibitisha shtaka bila kuacha shaka.

Alidai mahakama ilikosea kumtia hatiani kwa ushahidi ambao ulikuwa na mkanganyiko.

Rufani ilisikilizwa Februari 14, mwaka huu na mrufani aliwakilishwa na Wakili Jonas Kajiba na upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili Nashon Simon akisaidiana na Alfred Stephano.

Akiwasilisha hoja za rufani, Wakili Kajiba alidai upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha umri halisi wa binti, kuingiliwa kwa binti na utambuzi wa mrufani.

Alidai mama mzazi alisema binti ana miaka 11 na alipokuwa akihojiwa baada ya kutoa ushahidi alidai mwaka 2018 wakati binti anafanyiwa kitendo hicho alikuwa na umri wa miaka mitano.

"Hesabu ni rahisi, binti kazaliwa Februari 28, 2011 hadi mwaka 2018 alikuwa na umri wa miaka saba na si mitano.

"Binti katika ushahidi wake alijichanganya akaonyeaha tukio lilitokea mwaka 2018 na 2021, akadai aliitwa na mrufani akampe hela ya kununua viazi na katika mahojiano akadai alikuwa anampelekea viazi mama yake.

"Binti aliamua kukaa kimya au alishindwa kumtaja mrufani mwaka 2018 akamtaja mwaka 2021," alidai Wakili Kajiba.

Wakili Stephano, akijibu hoja hizo, alidai kuwa binti katika ushahidi wake alidai kazaliwa mwaka 2011, hivyo hadi tukio linatokea mwaka 2021 alikuwa na umri wa miaka 10.

Anadai mama yake kudai alikuwa na umri wa miaka 11 ni makosa ya kibinadamu na kuongeza kuwa hakuna mkanganyiko wa umri na kwamba binti alikuwa na umri chini ya miaka 18.

"Kutokana na Ushahidi, upande wa Jamhuri umethibitisha kwamba mrufani alimbaka binti. Naomba mahakama ione upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka dhidi ya mrufani na itupilie mbali rufani yake," alidai Stephano.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, ilisema tukio lilitokea kati ya mwaka 2018 na 2021 si binti wala upande wa Jamhuri anayejua siku halisi ya tukio lilipotendeka.

"Kuna mkanganyiko mwingi na matundu yaliyoachwa wazi yalipuuzwa na kuwekwa kando kana kwamba ilikuwa lazima kumtia hatiani mrufani.

"Hainishawishi kuamini kwamba binti alikaa kimya miaka miwili bila kumtaja mrufani kwa sababu alimtishia kumuua. Upande wa Jamhuri haukuimbia Mahakama kwa nini ilikuwa hivyo wakati mhanga (mwathirika) hakuwahi kutoka nje ya nchi.

"Kwa aina hii ya kiwango duni cha upelelezi, hakuna shaka kwamba hatia haikuwa na msingi. Mahakama inakubali rufani, inamwondolea hatia na adhabu mrufani.

"Mahakama inamwachia huru mrufani na kuamuru atolewe mara moja gerezani. Kama ataendelea kushikiliwa gerezani, basi kwa kwa kosa lingine, "alisema Jaji Laltaika.



Mbunge wa Muheza mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma maarufu kama Mwana FA akikabidhi zawadi ya mkungu wa ndizi wa futi sita kwa Makamu Mwenyekiti wa UVCCM Taifa na MNEC, Rehema Omary Sombi (wa tatu kushoto mbele), ambaye yupo katika ziara wilayani humo, jana. Wengine ni wanawake wajasiriamali. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Maoni ya wananchi dira ya maendeleo yaiva

**Na Joseph Mwendapole**

TUME ya Mipango imetangaza kuanza kukusanya maoni ya wananchi wa makundi mbalimbali kwa nchi nzima kuanzia mwezi huu kwa ajili ya kutengeneza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025-2050.

Ofisa Mkuu Mwandamizi wa Biashara na Ubunifu wa Tume hiyo, Dk. Crispin Ryakitimbo, alisema hayo jana wakati akitoa mada kwenye mkutano na wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Alisema watatumia mwezi huu wote kuzunguka mikoa yote kukusanya maoni kutoka kwa wananchi wa kawaida na wa makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali na wa dini kuchakata dira ya taifa.

Dk. Ryakitimbo alisema watafanya mahojiano na makundi kwa njia mbalimbali ikiwamo ya ana kwa ana, kwenye simu za viganjani na kutumia ujumbe kwenye simu za mkononi ili kuhakikisha wote wanafikiwa.

Alisema tayari walishakusanya maoni ya majaribio ambayo yalishawapia picha kamili kuhusu ufanisi wa nyenzo wanazotumia katika mchakato wa kukusanya maoni hao kutoka kwenye makundi mbalimbali.

"Tuna kituo chetu Dodoma ambacho tunapopata maoni yanaenda moja kwa moja kwenye kituo hicho kwaajili ya kufanya uchambuzi kwa hiyo hivi karibuni tunaanza rasmi sasa kukusanya maoni kwaajili ya dira ya taifa ya 2025-2050," alisema.

Alisema mchakato rasmi wa ukusanyaji maoni hayo unaweza kuchukua mwezi mmoja mpaka mwezi mmoja na nusu na kwamba wamejipanga kwa kanda ili kuweza kuwafikia wananchi wa mikoa yote.

"Tumegawa timu mbalimbali kwenye kanda, mfano kuna kanda inayojumuisha mikoa ya Morogoro, Pwani Lindi na Ruvuma, kanda inayojumuisha mikoa ya Arusha, kilimanjaro Arusha na Tanga, kuna kanda inayojumuisha Geita, Kagera, Mwanza na Mara tutagawana kwa mtindo huo kuhakikisha tunawafikia wananchi wote," alisema.

Alisema wakati wanaendelea kukusanya maoni hayo kwa kutumia vishkwambi mkusanya taarifa atatumia kifaa hicho kujiridhisha na taarifa alizokusanya na kisha kuwasilisha kwenye kituo chao cha Dodoma.

Mchakato huo wa kutengeneza Dira ya Taifa ya 2050, alisema unatarajiwa uwe umekamilika na dira kupatikana ufikapo mwaka 2026. Alitoa wito kwa wananchi wa makundi mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini kujitokeza kutoa maoni yao.

"Kwa kuwa dira hii inatakiwa ibebe maono ya watanzania wanataka Tanzania iweje kwa miaka 25 ijayo kama vile huduma bora za afya, miundombinu bora, elimu basi wahakikishe wanatoa maoni yako ya waachotaka kijumuishwe kwenye dira ya 2020-2050," alisema.

# Mafundi rukhsa ununuzi wa umma

**Na Joseph Mwendapole**

WABUNIFU wa mfumo wa kitaifa wa ununuzi wa kielektroniki (NeST), wameongeza kipengele kinachoruhusu mafundi stadi kushiriki rasmi katika ununuzi wa umma kwa kuomba zabuni.

Akizungumza na gazeti hili hivi karibuni, Meneja wa Usimamizi wa Mikataba kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Gilbert Kamnde, alisema kipengele hicho kitakuwa na mchango muhimu katika kufikia malengo yaliyowekwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

"Mafundi wa kawaida sasa wanaweza kushindana katika zabuni za ujenzi ambazo zilikusudiwa kupatikana kwa kila mtu kwa uwazi na bila ubaguzi kabisa," alisema.

Alisema dirisha hilo maalum lililoundwa linaruhusu mafundi stadi kujiandikisha katika kipengele hicho kwenye mfumo huo na kushiriki katika zabuni za ujenzi wa utaratibu wa Force Account tofauti na ilivyokuwa awali ambapo hakukuwa na utaratibu maalum wa ushirikishwaji huo na mashirika ya umma.

"Kukosekana kwa utaratibu mahsusi kulisababisha walengwa kutopata zabuni hizo na badala yake wakandarasi waliosajiliwa daraja la 6 au 5 wanashiriki na kupata zabuni zilizokusudiwa kwa ajili ya fedha za ndani," alisema Kamnde.

Alisema dosari iliyokuwopo inakinzana na matakwa ya Serikali kwamba kila mtanzania ana haki ya kushiriki katika manunuzi ya umma kwa haki.

Pia alisema ili mtu aweze kujiandikisha katika NeST kama fundi, mwombaji lazima awe na namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), leseni kwa wale ambao wana leseni au cheti kutoka taasisi zinazohusika na VETA.

Kamnde alisema kwa muda mfupi tangu dirisha hilo lifunguliwe NeST, zaidi ya mafundi 90 wamesajiliwa, jambo ambalo ni uthibitisho tosha kuwa mafundi wengi walikuwa wakisubiri kwa hamu kipengele hicho kwa ajili ya kuwatafutia mikataba katika mfumo wa manunuzi ya umma kwa imani.

Alisema PPRA inaendelea kuwashauri wazabuni wanaotarajiwa kujiandikisha kwenye NeST ili kutumia fursa zilizopo katika manunuzi ya umma, huku akisisitiza kuwa hakuna ununuzi wa umma utaofanyika nje ya NeST.

Alisema kifungo kisichozidi miaka mitatu jela au faini isiyozidi milioni 10 au vyote kwa pamoja vinamsubiri mtu yeyote atakayefanya manunuzi nje ya mfumo mpya.

## Hoja 120 kati ya 144 za CAG Singida hazijapatiwa majibu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

IMEELEZWA kuwa hoja 120 kati ya 444 zilizoibuliwa kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mkoani Singida kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 bado hazijafungwa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alibainisha hayo jana kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida wakati akielezea utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2023.

Alisema kati ya hoja 444 zilizoibuliwa na CAG ni 324 ambazo sawa na asilimia 72 ambazo zimejibiwa na kufungwa na kwamba katika kipimdi cha 2020/2021 hati safi zilitolewa kwa sekretarieti ya mkoa, halmashauri za Wilaya ya Manyoni, Mkalama, Ikungi, Itigi, Iramba, Singida DC na Manispaa ya Singida.

Serukamba alisema makisio ya bajeti ya mapato ya ndani ya Mkoa wa Singida yameongezeka kutoka Sh.bilioni 19.020 mwaka 2022/23 hadi kufikia Sh.bilioni 20.046 mwaka 2023/24.

Alisema hadi kufikia Desemba 2023 halmashauri za Mkoa wa Singida zilikuwa zimekusanya mapato huru ya ndani kwa asilimia 63.

Kuhusu pato la mkoa alisema limekuwa kutoka Sh.trilioni 2.8 hadi kufiki Sh.trilioni 3.2 mwaka 2022 na wastani wa pato la kila mtu nao umeongezeka kutoka Sh. milioni 1.6 mwaka 2020 hadi kufikia Sh.milioni 1.7 mwaka 2021.

Serukamba alisema utengaji wa fedha za mapato ya ndani kwenda kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Sh.milioni 576 .660 zimepelekwa kwenye mfuko huo sawa na asilimia 56 ya makusanyo ya Julai hadi Desemba 2023.

Alisema kati ya fedha hizo zilizotolewa Sh.milioni 394.558 zimerejeshwa sawa na asilimia 62 ya lengo ambapo vikundi vya wanawake zimerejeshwa Sh.milioni 223.270, vijana Sh.milioni 133.962 na watu wenye ulemavu zimerejeshwa Sh.milioni 37.325.

Kuhusu utekelezaji wa TASAF mkoani Singida, alisema Sh.bilioni 7.014 zililipwa kama ruzuku kwa walengwa 56,948 katika vijiji 512.

# Mikoa sita vinara utoaji huduma chakula shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja mikoa sita ambayo imefanikiwa kutoa huduma ya chakula shuleni, ili kuchochea ubora na ufaulu kwa wanafunzi.

Mikoa hiyo ni Njombe, Kilimanjaro, Arusha, Pwani, Iringa, Manyara ambayo huduma hiyo inapatikana kwa zaidi ya asilimia 80.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk.Franklin Rwezimula, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya Siku ya Afrika ya Chakula Shuleni iliyoandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau kutoka Shirika la Global Communities kupitia mradi wa Pamoja Tuwalishe na Shirika la Sanku.

Alisema kukosekana kwa chakula shuleni kunachangia utoro wa rejareja kwa wanafunzi na wengine kukatisha masomo na kutokana na hali hiyo serikali imeweka mwongozo wa upatikanaji wa chakula shuleni unaolenga kushirikiana na jamii kuchangia upatikanaji wa chakula.

Alisema maadhimisho hayo ni ya kwanza kufanyika nchini na ni kwa mstakabali wa wanafunzi wanaosoma shule za awali, msingi na sekondari.

"Lengo ni kuhamasisha jamii, wadau na serikali kuweka mikakati ya kutekeleza afua za lishe shuleni, yapo madhara makubwa ya kukosekana kwa chakula kuwa ni njaa, usikivu, utoro wa rejereja na kukatisha masomo,"alisema.

Pia alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu na kwamba upatikanaji wa matokeo mazuri ya elimu hutegemea afya bora kwa wanafunzi.

"Sera ya Elimu ya Mwaka 2023 inafafanua wadau kushirikiana na serikali kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa huduma muhimu ikiwamo chakula na majisafi shuleni na vyuoni," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi Uendeshaji Sera Elimu Msingi wa Wizara hiyo, Victor Bwindiki, aliomba wadau kutambua umuhimu wa chakula shuleni kwa kuwa unachochea ubora wa elimu na ufaulu kwa wanafunzi. Alisema wanafunzi bila afya bora wanakuwa na usikivu hafifu.

Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Global Communities wanaotekeleza mradi wa Pamoja Tuwasilishe, Vick Macha, alisema wamekuwa wakitekeleza kwa miaka 10 utoaji chakula shuleni kwa mikoa ya Dodoma na Mara na kuahidi kuendelea kushirikiana na serikali kufanikisha mwongozo wa kutoa chakula shuleni.

Mratibu wa masuala ya lishe wa wizara hiyo, Grace Shileringo, alisema mwanfunzi hawezi kujifunza na kusoma vizuri bila kuwa na lishe na kutoa wito kwa wazazi kuchangia chakula shuleni.



Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha kuzalisha dawa asili cha Billy Formula Power kilichopo Manispaa ya Moshi, Danny Kyauka, akionyesha dawa hiyo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma jana, inayotumika kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa figo, iliyofanyiwa utafiti na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA), kwa ufadhili wa serikali na kuonyesha matokeo chanya kwa ngazi ya wanyama. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Serikali yapewa mbinu kupunguza gharama matibabu ugonjwa wa figo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na gharama kubwa za matibabu ya ugonjwa wa figo ndani na nje ya nchi, Serikali imeshauriwa kuwatumia wataalam wa tiba za asili kufanya utafiti ambao utasaidia kupatikana kwa dawa zitakazotumika kutibu tatizo hilo.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha tiba ya asili cha Billy Fomula Power kilichopo mkoani Moshi, Danny Kyauka kinachozalisha dawa aina ya Billy Formula Power inayotumika kutibu ugonjwa wa figo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya kupokea majibu ya utafiti wa awali wa dawa ya Billy Formula Power 2023 uliyofanywa na Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) ngazi ya wanyama, alisema hivi sasa gharama za matibabu ya ugonjwa wa figo nchini zipo juu hivyo ipo haja kwa serikali kushirikiana na wataalam wa tiba ya asili kufanya utafiti ambazo zitakuwa na tija.

"Naomba serikali ilibebe jambo hili ili kuwezesha tafiti kama hizi ambazo zitasaidia kupatikana kwa dawa za kutibu magonjwa mbalimbali kupitia utajiri wa mimea tiba tuliyonayo nchini.

"Hii ni dhahabu ambayo kama leo tutaitumia vizuri itakuwa na msaada mkubwa sana kwenye matibabu, wenzetu China tiba asili ni kipaumbele chao lakini pia India ambao ndiyo sisi tunapeleka kwa wingi watu wetu hivi sasa wapo katika mkakati wa kujenga hospitali kubwa ya tiba asili" alisema Kyauka

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuwezesha utafiti huo ambao umefanywa na Chuo cha SUA na vyuo vingine ambavyo vimeshiriki kukamilisha kazi hiyo.

"Lakini pia nampongeza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Naibu wake Dk. Godwin Mollel kwa kunisaidia kupata matokeo ya utafiti huu na naiomba serikali majibu ya utafiti huu yawekwe bayana kwa umma" alisema.

Barua ya majibu ya utafii huo iliyoanadikwa na Dk. Mwinyokondo Amir ilisema wizara hiyo imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za tiba asili kwa kuhakikisha ubora wa huduma na dawa zinazotolewa zipo katika usalama wa walaji.

Alisema kwa mujibu wa barua hiyo wizara inamjulisha kuwa dawa ya Billy Formula Power miongoni mwa dawa iliyofanyiwa utafiti wa awali kwa wanyama na majibu yametoka.



# Waomba elimu kufahamu kazi ya Tume ya Maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja, wameiomba Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoa elimu mara kwa mara ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa tume hiyo nchini.

Waliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati maofisa wa tume hiyo walipofanya ziara ya kutoa elimu kwa wananchi wa mkoa huo.

Bahati Bakari miongoni mwa wananchi hao alisema uelewa kwa jamii, juu ya majukumu ya tume hiyo bado ni mdogo, jambo ambalo linasababisha kuchelewa kufikia malengo mazuri yaliyopangwa na Serikali.

Aidha alisema endapo jamii itakua na uelewa wa kutosha juu ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, itawafahamu viongozi wanaokiuka maadili pamoja na kujengeka ujasiri wa kutoa taarifa za viongozi hao sehemu husika ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Hata hivyo wananchi hao waliitaka tume hiyo, kuimarisha ulinzi na usalama kwa wanaotoa taarifa pamoja na kutoa msisitizo kwa wananchi ili jamii iendelee kuwafichua viongozi wanaokwenda kinyume na maadili.

Ali Kahmia aliwataka wazazi na walezi kushirikiana katika malezi ya watoto kwa kufuata misingi ya maadili ili kuepusha kuwa na viongozi wasio na maadili hapo baadae.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma katika Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Halima Jumbe Saidi alisema tume hiyo inawajibu wa kutunza siri zinazotolewa na wananchi sambamba na kufanyakazi kwa ushirikiano kati ya tume hiyo na wananchi ili kuhakikisha haki zinapatikana.

Pia alisema tume itendela kutoa elimu ili jamii ipate uelewa na kutoa taarifa za viongozi wanaokwenda kinyume na maadili na miongoni mwa majukumu mengine ya tume hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kupokea malalamiko ya viongozi wanaokwenda kinyume na maadili.

"Serikali imeweka taasisi mbalimbali za kutoa elimu ya maadili ikiwemo tume hii , Ofisi ya Mufti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kuhakikisha jamii yote inaishi kimaadili mema yanayokubalika katika jamii." alisema Halima.

Hata hivyo aliwasisitiza wananchi kufika Ofisi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupeleleka malalamiko dhidi ya viongozi wanaowatuhumu kufanya ubadhirifu na kuahidi kuwa tume hiyo, itaendelea kusikiliza madai ya mwananchi yoyote dhidi ya kiongozi anakwenda kinyume na maadili kwa usiri.

Kwa upande wake ofisa kutoka tume hiyo, Habib Said Mohammed alisema kuna baadhi ya viongozi wanadaiwa wanajihusisha na vitendo vya rushwa, kutelekeza familia zao, kutumia mali za umma kwa maslahi yao na kutumia madaraka vibaya jambo ambalo kinyume na maadili ya tume hiyo.

Akitaja adhabu kwa viongozi watakaobainika kwenda kinyume na maadili ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa kazi, kukatwa mshahara na kushauriwa kujiuzulu kulingana na kosa alilofanya.

Tume ya maadili ya viongozi wa umma imetoa elimu katika shehia mbalimbali za Mkoa wa Kusini Unguja ikiwemo Shehia ya Kijini, Nganani na Kiongoni na kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni pamoja na Shehia ya Kitope, Matetema na Kwagube.

# Serikali yapiga marufuku muziki kumbi za starehe msiba wa Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUFUATIA kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga marufuku upigaji wa muziki wa aina yoyote katika kumbi za starehe na burudani.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu, Dk. Omar Abdalla Adam alitoa katazo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema hatua hiyo imekuja baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kutangaza kifo cha Rais huyo mstaafu na kutoa siku saba za maombolezo.

Alisema kwa mujibu wa Kifungu 8(1), (d) cha Sheria Namba 7 ya 2015 ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar, Baraza limepiga marufuku shughuli zote za sanaa na burudani katika maeneo ya starehe yakiwemo maeneo ya kijamii, hoteli, kumbi na baa.

Katibu huyo aliwataka wananchi kushirikiana katika kipindi hiki cha msiba kufuata agizo hilo, kwa kutopiga ngoma katika shughuli zote ikiwemo muziki au sherehe za harusi zilizoambatana na muziki.

"Harusi kama utamaduni wetu ziendelee kufanyika kama kawaida katika familia zetu isipokuwa hakutakuwa na upigaji wa ngoma na sherehe nyingine kutokana na utamaduni, mila na silka zetu," alisema Dk. Omar.

Alisema kuwa tukio hilo ni la kitaifa, hivyo atakaekwenda kinyume na tamko hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kufungwa kwa muda wa miezi sita ama kulipa faini ya Sh.milioni moja.

Aidha alisema baraza litafanya doria katika kumbi na sehemu zote za starehe ili kuwabaini watakaokwenda kinyume na agizo hilo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Hata hivyo aliwashauri wale ambao wameshaweka oda kwa ajili ya shughuli katika kipindi hiki kuwarejeshea fedha zao ama kufanya mazungumzo baina yao, ili kupisha siku za maombolezi na baadae kuendelea na shughuli hizo.

Al-hajj Mwinyi alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Mzena jijini Dar-es-Salaam na atazikwa leo kijijini kwao Mangapwani Wilaya ya Kaskazini "B" Mkoa wa Kaskazini Unguja.



Polisi Kata ya Njianjema wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, George Mhina akichangia hoja katika kikao cha kujadili mikakati ya kuimarisha ulinzi katika kata tano za Dunda, Magomeni, Nianjema, Kisutu na Kiromo, wilayani humo juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yaomba msaada mapambano dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman amewataka wanachi kutoa taarifa kwa wanaoingiza dawa za kulevya nchini, ili kudhibitiwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Aliyasema hayo wakati akiwasilisha Ripoti ya Dawa za Kulevya Zanzibar ya Mwaka 2022-2023 katika Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Alisema wizara itatoa zawadi maalum kwa watakaotoa taarifa hizo.

Alisema bado serikali haijaweza kuwakamata waingizaji wakubwa wa dawa za kulevya, hivyo aliwaomba wananchi kuunga mkono mikakati iliowekwa na serikali.


Aidha aliwapongeza wananchi kwa kutoa taarifa ya dawa za kulevya na kutokata tamaa kwa serikali kwa sababu serikali ipo pamoja na wananchi hao katika kuwanusuru na janga hilo.

Hata hivyo aliwataka wananchi kufuatilia watoto wao waliopo shuleni na maeneo mengine ili kuwanusuru na tatizo hilo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Maryam Thani Juma aliitaka Serikali kuzidi kuchukuwa juhudi ya kupambana na wahalifu wanaoingiza dawa za kulevya nchini, sambamba na kuipongeza Serikali kwa kutekeleza kwa vitendo mikakati walioipanga.

Wakichangia ripoti hiyo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walitaka kuongezewa bajeti Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ili kufanya kazi kwa ufanisi na kufikia malengo yaliokusudiwa katika kupambana na kuthibiti vitendo hivyo.

Pia waliitaka Serikali kuangalia uwezekano wa kuipatia vifaa vya kisasa na vya kutosha mamlaka hiyo kwa lengo la kudhibiti vizuri maeneo husika na kudhibiti dawa hizo zisiingie nchini.



# BEYONCE

UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI MACHI 2, 2024



# MWINYI ALIINUA BURUDANI

Ni msiba wa Watanzania wote. Ndivyo unavyoweza kusema baada ya juzi saa 11:30 jioni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alipotangaza rasmi kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, aliyeiongoza nchini kuanzia mwaka 1985 hadi 1995, akichukua kijiti kutoka kwa Rais wa Kwanza, Julius Kambarage Nyerere.

Ni kiongozi aliyefanya mambo mengi sana mazuri, akiwa kipenzi cha wananchi wake kiasi cha kumpachika jina na kumwita 'Mzee Rukhsa', lakini hapa tunamuangazia katika nyanja za sanaa na burudani.

Tunaweza kusema baada ya Mwalimu Nyerere, Mzee Mwinyi naye aliiwezesha sanaa ya burudani kukua na kufanya vyema sana enzi zake.

Ikumbukwe ni kipindi chake ndipo bendi za muziki wa dansi zilivyozidi kushamiri zikiwemo Juwata Jazz Band, 'Msondo Ngoma' na DDC Mlimani Orchestra, Sikinde Ngoma ya Ukae' ambao ni wapinzani wa jadi.

Mwaka 1985 ambao Mwinyi anaingia madarakani ndiyo mwaka ambao Hassan Rehani Bitchuka na Muhidini Maalim Gurumo walipoondoka Sikinde na kwenda kujiunga na bendi ya Orchestra Safari Sound, wakitumia mtindo wa Ndekule.

Bendi hiyo ilileta chachu na kuufanya muziki wa dansi kuwa juu na ushindani mkali.

Ni kipindi cha utawala wake ambapo bendi ya Vijana Jazz iliyokuwa ikimilikiwa na Umoja wa Vijana Tanzania, ilipopata vyombo vipya aina ya Ranger kutoka nchini Italia na kuifanya kuwa tishio kwa bendi kubwa, ikiwemo hata kutwaa baadhi ya wanamuziki wake, mfano ilimchukua Ally Jamwaka kutoka Sikinde na Suleiman Mbwembwe kutoka Msondo.

Kipindi cha utawala wa Mwinyi, ndicho ambacho taarab ilikupanda na kuwa kwenye kiwango cha hali ya juu kukiwa na makundi mengi kama Bima Taarab, na JKT Taarab iliyorekodi nyimbo kama 'Njiwa','Ukewenza', 'Kupeana na Kikoa', 'Chura' na zingine nyingi.

BASI SAWA

## Baba Levo aguswa na msiba



KATIKA ukurasa wake rasmi wa msanii wa muziki wa Bongo fleva, Baba Levo, ameweka picha ya rais mstaafu mzee Ally Hassan Mwinyi na kumuombea apumzike kwa amani.

Baba Levo katika chapisho lake hilo aliambatanisha na emoji zinazoonyesha akilia kama ishara ya kuumizwa na kifo cha kiongozi huyo ambaye alikuwa kama alama ya umoja kwa wananchi wa Tanzania.

Mzee Mwinyi amekuwa kipenzi cha wasanii wengi nchini kutokana na utawala wake kusimamia kikamilifu ukuaji wa sekta ya burudani.

## Vanillah asema taifa limehuzunika

MSANII anayekuja kwa kasi kutoka lebo ya Kings Music, Vanillah, amekuwa miongoni mwa wanamuziki wachanga walioguswa na kifo cha Mzee Mwinyi.

Katika ujumbe wake wa rambirambi kupitia ukurasa wake wa Instagram, Vannilah amemtakia pumziko jema na amani na kueleza kifo chake kimewahuzunisha Watanzania wote.

“Mzee wetu Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, sisi kama Kings music tunatoa pole kwa Taifa na familia kwa ujumla,” ameandika Vanillah.





# MARIOO AMWAGA MACHOZI

MKALI wa muziki wa Amapiano nchini, Marioo, amemkumbuka rais mstaafu Ally Hassan Mwinyi kama mtu mnyenyekevu na asiyetaka kujikweza licha ya kuwa na hadhi ya juu.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Marioo ameweka video fupi ikimuonyesha hayati Mzee Mwinyi, akizungumzia namna ya viongozi kuonyesha wema kwa kila mtu na kuwa hadithi nzuri hapa duniani.

Marioo ameambatanisha na ujumbe unaosema “Pumzika kwa Amani Mzee wetu,”.



# Diamond, Zuchu wamlilia Mwinyi

WASANII wa Bongo Fleva kutoka lebo ya WCB, wakiongozwa na bosi wao Diamond Platnumz, nao wameungana na Watanzania kuomboleza kifo cha rais wa pili wa Tanzania, Mzee Ally Hassan Mwinyi kilichotokea juzi.

Katika kurasa zao za Instagram, wanamuziki Diamond na Zuchu, wamesema kiongozi huyo amefanya mengi katika utawala wake na mpaka sasa bado yanaendelea kuishi.

“Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi amina @ ameandika Diamond huku akiambatanisha picha ya kiongozi huyo.

# WAKALI WA MAGITA YA KATI BONGO

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA muziki wa wa laivu ili uwe bora kunatakiwa kuwa na magita matatu au manne.

Hayo ni ‘solo’, ‘second solo’ au Wakongomani wanaliita ‘mini solo’, ‘rhythm’ na ‘bass’.

Ili muziki uwe bora na usikike vizuri kwenye masikio ya msikilizaji, unatakiwa uwe na idadi hii ya magitaa, au kama yakipumgua yawe matatu.

Leo tunaaangalia wapiga magitaa ya ‘rhythm’, ambalo linasaidiana na gitaa ongozi la solo, na ndilo linaloongoza muziki mzima.

Ndilo linaloongoza njia nzima ya wimbo husika kwa waimbaji na wapiga vyombo.

Cha ajabu ni kwamba wasanii wa bongo fleva, pamoja na siku hizi baadhi kutumia gitaa la solo, lakini hakuna anayekumbuka kutumia gitaa hilo. Wafuatao ni wapiga magitaa ya ‘rhythm’ walioondokea kuwa maarufu nchini.

**1. Abdallah Gama-Bima Lee**

Ni mpiga gitaa la rhythm bora kabisa kuwahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania. Umaarufu wake hasa umetokana na nyimbo nyingi alizopiga akiwa na DDC Mlimani Park Orchestra.

Kabla ya hapo aliwahi kupigia bendi za Safari Trippers, Dar International na alipotoka Sikinde alikwenda kupigia bendi ya Bima Lee. Gama bado yupo na anaendelea na muziki.

**2. Mustapha Hamisi ‘Pishuu’-Msondo**

Baada ya kuondoka kwa Abdallah Omari ‘Dulla’ aliyekumbwa kwenye wimbi la wanamuziki mwenda Sikinde, Msondo ilimtafuta mpiga rhythm bora bila mafanikio.

Lakini kwa mastaajabu ya wengi walimpata kijana mmoja Mustapha Hamisi, ambaye aliliziba kikamilifu na kuwa mmoja wa wapiga rhthm bora kabisa kuwahi kutokea nchini Tanzania.

Mashabiki wa Msondo wanampachika jina la ‘Pishuu’ wakimfananisha na mpiga rhythm mmoja wa bendi ya Shamashama ya nchini Congo DR mwenye jina hilo.

**3. Mwarami Said-Sikinde**

Sikinde ilibahatika kumpata mpiga rhythm mmoja matata sana aitwaye Mwarami Said, na mashabiki wakamuongeza jina lingine akawa ‘Golden Finger.’

Alikuwa mwanamuziki wa DDC Mlimani Park Orchestra ambao walimchukua kutoka kwenye bendi ya JKT Kimbunga Stereo. Huyu hakuwa mahiri kwenye upigaji tu, lakini alikuwa mkali kwenye kutunga nyimbo pia.

**4. Kassim Karuona-Tabora Jazz**

Bendi ya Tabora Jazz ilikuwa mahiri mno kwa staili yake ya kupiga muziki halafu unazimwa na kuachiwa mpiga rhythm pekee na drums wakihenyeshana.

Kassim Karuona alipata umaarufu mkubwa kwenye bendi hiyo kutokana na umahiri wake mkubwa wa kupiga gitaa hilo.

Ukiangalia hata wimbo wa ‘Dada Asha’ ulirudiwa na bendi maarufu ya Congo, Soukouss Stars, lakini mpiga rhythm wao maarufu alikuwa marehemu Lokassa wa Mbongo.

**5. Ally Said-Urafiki Jazz**

Moja kati ya wapiga magitaa ya ‘rhythm’ ambao historia ya muziki wa Tanzania haimtendei haki ni Ally Said.

Hatajwi sana na wachambuzi wa muziki na mashabiki, lakini ukisikiliza nyimbo nyingi alizopiga utagundua kuwa hana mfano wake.

Nyimbo nyingi za Urafiki Jazz kuna vipande vimeachiwa gitaa la rhythm litambae na yeye ndiye aliyepiga nyimbo nyingi kama ‘Asma’, ‘Paulina’, ‘Unguja na Tanga’, ‘Mauji wa Soweto’, Rudisha Pete Lucy’ na nyingine ambazo amepiga kwa ustadi mkubwa.

FILAMU

# Shakira: Mungu kakupa mume

**Na Adam Fungamwango**

LILILOPANGWA na Mungu binadamu hawezi kupangua. Binadamu hata siku moja hawezi kupangua kitu kilichopangwa na Mungu.

Unaweza kutaka kufanya hivi, lakini Mungu akabadilisha na kukupa kingine ambacho yeye anataka kiwe.

Unaweza kutaka kumuoa au kuolewa na fulani, lakini kumbe Mungu kasema wala si yeye, yupo mwingine kabisa.

Pia Mungu anaweza kumpa riziki, mtu amtakae. Katika filamu hii tunaona msichana ambaye aliletewa barua mbili kwenye kijiji chao. Kilichotokea ni kwamba akaenda kuolewa na mtu mwingine kabisa ambaye hata yeye mwenyewe hakupanga hivyo. Na muoaji wala hakuota kama anaweza kumpata mke huyo.

Imechezwa na Natalia Francis, kama Shakira Abdul Sharmaa, yeye akaigiza kama mzee Mboko Ernest Hassan, amecheza kama Ibra, Rajab Juma yeye akawa, Tesha, wengine ni Suraj Afuraha, Dotto Jeylos.

Shakira ni msichana mrembo anayeishi na bibi na babu yake baada ya wazazi wake kufariki dunia.

Ana mpenzi wake anaitwa Tesha, lakini kuna mzee mmoja hivi anaitwa Mboko, alivutiwa na uzuri wa binti huyo, akaamua kupeleka posa.

Babu na bibi yake wakakubali, lakini yeye alikataa, na akaenda moja kwa moja kwa mpenzi wake Tesha kumwambia na yeye apeleke posa ili aichague yake na kuikataa ya mzee Mboko.

Akafanya hivyo, Shakira akaikubali ya Tesha na kuikataa ya mzee Mboko. Siku chache baadaye, Shakira akaota amebakwa, lakini baada ya wiki kadhaa alionekana kuwa na ujauzito.

Hakuna anayeamini kuwa ujauzito huo ni wa kwenye ndoto, si babu yake, bibi wala mpenzi wake Tesha.

Walezi wakamfukuza, na Tesha pia akamkataa. Akaondoka kusikojulikana na kuokotwa porini kwenye vijiji vya mbali na bibi mmoja ambaye alimchukua na kumpeleka nyumbani kwake.

Akamtibia, alipopona akamhadithia yote. Bibi huyo akamwambia hiyo ni michezo ya watu wabaya, hivyo akampa dawa, ujauzito huo wa kichawi ukatoweka. Ilikuwa kazi ya mzee Mboko, baada ya kukataliwa.

Wakati huo huo, bibi yo alikuwa na kijana wake aitwaye Ibra ambaye kwa siku zote alipokuwa akiishi hapo walitokea kupendana.

Baada ya kupona, Shakira akarejea kwao, ikiwa ni baada ya miezi mingi kupita. Akapokewa vizuri na bibi na babu yake ambao walihadithiwa kila kitu.

Baada ya siku chache ikaletwa barua ya posa kutoka kwa kina Ibra. Walezi wake akamuuliza kama anamfahamu. Naam! Akakubali kuwa huyo ndiye haswa mume aliyepangiwa na Mungu. Si Tesha wala mzee Mboko.





# Beyonce yulee kileleni

MWANAMUZIKI nyota wa Marekani, Beyonce Knowles, amekuwa na furaha baada ya wimbo wake mpya 'Texas Hold 'Em' kushika namba moja katika chati maarufu duniani ya Billboard.

Wimbo huo ambao umepata maarufu ulianza kushika nafasi ya pili wiki iliyopita, na baadae ulipanda hadi nafasi ya kwanza katika wiki ya pili sasa.

Chati ya Billboard Hot 100 ndiyo inaheshimika katika tasnia ya muziki nchini Marekani kutokana na vigezo vya viwango vya juu vya mauzo, kimwili na kidijitali, uchezaji wa redio na utiririshaji mtandaoni.



## Fireboy afichua ya kale

NYOTA wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Fireboy DML, amefichua kuwa alikuwa na furaha wakati alipomchumbia mwanamuziki maarufu wa Marekani, Madona.

Mwimbaji huyo alitoa siri hiyo wakati alipozungumza na jarida la Billboard kuhusu kupanda kwake umaarufu.

Fireboy, ambaye ni shabiki wa mwimbaji huyo wa kibao cha La Isla Bonita, alisisitiza kuwa siku hiyo ilikuwa muhimu kwake na kwamba hataisahau.

"Sitasema kila kitu lakini niliingia kwenye penzi la Madonna na niseme ukweli kwamba ilikuwa siku ya kukumbukwa zaidi kwangu ambayo ninaishi nayo," alisema huku akitabasamu.

## Zubby kwa mkwara huo noma!

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Zubby Michael, amejigamba kwamba yeye ndiye msanii mkubwa na tajiri barani Afrika.

Msanii huyo wa filamu za Kinigeria, amesema kutokana na kuwa na ukwasi wa kifedha na kwamba anaweza kuwalipa waigizaji wenzake kama Timini Egbuson.

Maoni yake hayo yaliibua malumbano makali kati yake na mwigizaji mwenzake Timini kwenye kipindi cha televisheni ambacho kimewafanya watu kutoa maoni tofauti kuhusu kauli hiyo.







## Portable pesa zote unapeleka wapi?

MWIMBAJI maarufu wa muziki wa Pop kutoka Nigeria, Portable, ameibua mjadala baada ya kuonekana akibeba lundo la pesa za noti kwenye mikono yake.

Video yake ambayo imemuonyesha akibeba pesa hizo zilisambaa katika mitandao ya kijamii na kusababisha mashabiki wake kuwa na hisia tofauti.

Hata hivyo, Portable mwenyewe ametoa ufafanuzi kwamba pesa hizo zimetokana na shoo zake alizofanya nchini Uingereza katika ziara yake ya muziki.

## 2Baba anakumbuka mengi

MWANAMUZIKI mkongwe nchini Nigeria, Innocent Idibia maarufu kama 2Baba, amesema alipata shida wakati akitafuta njia ya kutoka kimuziki.

Akizungumza katika mjadala kuhusu wasanii waliofungua njia katika muziki nchini humo, 2Baba amesema msanii pekee aliyemuunga mkono ni Daddy Showkey alivyoonyesha kumuunga mkono kwenye tamasha moja lililofanyika miaka ya 90.

Alikumbuka jinsi yeye na mwanamuziki mwenzake Blackface, waliponyanyaswa kwenye onyesho kabla ya Baba Showkey kuingia na kurekebisha hali hiyo.





# Serikali yafanya kampeni kudhibiti usubi, kichocho, minyoo

**Na Steven William,** MUHEZA

MARADHI ya usubi, kichocho na minyoo ya tumbo inayotishia mustakabali wa afya za wakazi wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, umeiamsha Wizara ya Afya kuendesha kampeni maalum ya kuwakinga wananchi hao na magonjwa hayo.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele wa Wilaya hiyo, Julius Mgeni, maradhi hayo yamewasababishia baadhi ya wakazi wake ulemavu wa kudumu kutokana na kukosa kinga.

Mgeni alikuwa akizungumza jana katika kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi cha Wilaya hiyo.

"Malengo yetu ni kutoa dawa ya usubi kwa walengwa 200,258. dawa za kichocho kwa wanafunzi 10,393 walioko katika shule 26 za kata nane na dawa za minyoo kwa walengwa 55,097," alisema.

Alisema dawa za ugonjwa wa kichocho zinatolewa kwenye shule za msingi katika kata za Zirai, Kwakifua, Pande Darajani, Mbomole, Misozwe na Tingeni.

Nyingine ni Kwafungo na Misalai na dawa za minyoo ya tumbo, zitatolewa katika shule zote 126 za msingi zilizoko wilayani Muheza.

Ofisa Tarafa ya Muheza, Japheti Ndagamusu, aliyemwakilisha mkuu wa wilaya hiyo, Juma Irando, alisema serikali itahakikisha wananchi wake wanapata dawa ambazo zitawasaidia kutopata ulemavu, utakaotokana na usubi pamoja na magonjwa minyoo ya tumbo.

Mkuu wa Divisheni ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, alisema kampeni hiyo ni muhimu, huku akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupata tiba hiyo.

# Idadi ya vijana kutoka Moshi wanaokimbilia mjini yaongezeka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIJIJI vinne vya Korini Kati, Korini Juu, Korini Kusini naTema vilivyoko Kata ya Mbokomu, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, baadhi ya nyumba zimegeuka magofu baada ya idadi kubwa ya vijana kukimbilia mijini kutafuta maisha wakisingizia kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Korini Juu, wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Polisi kilichojengwa nguvu za wazawa wa Mbokomu waishio Jijini Dar es Salaam cha New Mbokomu Development Group, Wenseslaus Mushi, alisema kukosekana kwa huduma hizo kumeifanya kata hiyo kuachwa nyuma kimaendeleo.

"Sasa hivi ukija na Sh. milioni moja hapa Mbokomu, unaweza kulala na njaa. Nilikuja na hiyo pesa mfukoni nikawa naziangalia tu hakuna mahali pa kula, kutumia pesa, hakuna bucha, hakuna hoteli ni mpaka uende Kiborloni.

Wahalifu wote wanatoka Mbokomu. Ukienda mahakama za Old Moshi nusu ya wahalifu pale wanatoka Mbokomu. Tukasema tuwawekee Kituo cha Polisi hapa karibu na vilevile tukipata nafasi (ardhi) tunajenga Mahakama ya Mwanzo hapa hapa Mbokomu."

Kutokana na changamoto hiyo, Mushi alisema wazawa hao waliamua kuja na wazo la kujenga kituo kidogo cha polisi Mbokomu pamoja na nyumba ya kuishi askari polisi, ambavyo vimewagharimu Sh. milioni 35.

Alisema kituo cha polisi pekee kimejengwa kwa Sh. milioni 22.5, kikiwa na mahabusu ya kisasa za wanaume na wanawake, ofisi ya mkuu wa kituo, kaunta na choo cha ndani cha kisasa cha askari.

Wakati nyumba ya askari wa kituo hicho ya vyumba viwili vyenye kila kitu, ambayo itatumiwa na askari ambao hawana familia, imegharimu Sh. milioni 12.5.

Akizungumza na wakazi wa Mbokomu, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa (SACP), aliwataka wakazi wa vijiji hivyo kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye kata yao.

"Ninyi wana Mbokomu, utalii utawabeba, Kili Marathon juzi ilikuwa na watu zaidi ya 20,000 kulikuwa hakuna hoteli za kutosha. Jengeni hoteli na nyumba za kisasa za kulaza wageni, hapa ni karibu sana na mji wa Moshi.

...Kujenga kituo cha polisi sio kipimo cha kumaliza uhalifu kama wewe mwenyewe kwenye mindset hautabadilika. Nimeona hapa viongozi wenyewe mmeanza kulumbana, ni kweli chanzo cha uhalifu ni matumizi ya kuzidi.

Tumesikia kuna ulevi wa kupitiliza, ulevi wa kupindukia. Tengenezeni sheria ndogo za kuweka muda wa kunywa pombe. Kwa sababu tusipokuwa na mipaka ya muda, sisi wenyewe tutageuka kuwa tatizo."

Zaidi aliongeza: "Haiingii akilini asubuhi kijana anaonekana amelewa, kijana mdogo anaonekana ana umri mkubwa, amezeeka kuliko hata sisi wazee. Kumbe ni matumizi ya ovyo ya gongo.

"Nimeambiwa hapa kuna baadhi ya nyumba zimekuwa ni magofu. Bora ziwe magofu kwa sababu ya maendeleo lakini eti kuna kuwa hakuna hoteli, hakuna mahali pa kula cha kula kwa sababu ya uhalifu. Hiyo haikubaliki.

"Jamani mrudi nyumbani muwekeze Mbokomu, kwa sababu mama yako ni ardhi ya Mbokomu hutapata ardhi nyingine inaitwa Mbokomu kama utaiondoa amani na uwekezaji."

Kutokana na tishio la uhalifu, Kamanda Maigwa alimwagiza Mkaguzi wa Kata wa Polisi, Peter Mrwanda, kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi kuanzia sasa katika kata hiyo.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Erasto Mhina akifungua kikao cha Baraza la Madiwani, kilichojadili mambo mbalimbali ya miradi ya maendeleo, juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Juma Mhina na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Salimu Sechambo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vinyonga wa pembe tatu waanza kurejea Hifadhi ya Amani

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

VIUMBE hai adimu waliokuwa katika hatari ya kupotea, ikiwamo vinyonga wa pembe tatu wanaopatikana zaidi katika ikolojia ya Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani, wameanza kurejea tena, baada ya wananchi wa vijiji 20 vya Wilaya ya Muheza ambavyo vinauzunguka kujumuishwa katika shughuli za uhifadhi.

Jana, Kaimu Mhifadhi wa Hifadhi hiyo, Nikundiwe Majoya, alisema vinyonga hao walianza kupotea kutokana na kukithiri kwa shughuli za binadamu na uharibifu wa mazingira yao ya asili.

"Hivi sasa wananchi hawa hawaingii tena msituni kufanya shughuli mbalimbali ambazo siyo rafiki katika uhifadhi wa mazingira. Hii ni kwa sababu wananufaika na ajira, ikiwemo za usafishaji wa mipaka, uboreshaji wa barabara za kupita watalii pamoja na miundombinu mingine ya kuvutia utalii.

"Tunaona maboresho ya viumbe hai, yanazidi kuboreshwa na hata vilivyokuwa vimetoweka awali, sasa vimerejea katika hali yake ya kawaida; hasa ndege na viumbe vingine kama vinyonga, ambao wanapatikana katika msitu huu."

Aidha, alisema kuwa wananchi wa vijiji hivyo hivi sasa wanawezeshwa kwa kupewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi rafiki, ikiwemo ya upandaji miti, utengenezaji majiko sanifu, ufugaji wa samaki na nyuki ili kupunguza kasi ya uvunaji wa rasilimali za misitu kama kuni kwa ajili ya kupikia na ukataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na kupasua mbao.

Alisema miradi hiyo inafadhiliwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF), umesaidia kuongeza mapato ya hifadhi hiyo kutoka Sh. milioni 30 kati ya mwaka 2022/2023 hadi Sh. milioni 40 mwaka 2023/2024.

Idadi ya watalii katika kipindi hicho, imeongezeka kutoka 3,000 hadi kufikia 4,000.

Mmoja wa wanufaika wa ajira hizo, Mrisho Nzota, Mkazi wa Kijiji cha Mikwinini, alisema kutokana na elimu ya uhifadhi waliyopewa imewasaidia kutambua umuhimu wa utunzaji wa mazingira, huku ajira hizo zikiwapa kipato kinachowawezesha kuhudumia familia zao.

Wakati, Daudi Tofio, mkazi wa Kijiji cha Kisiwani, alisema moja ya mambo wanayofurahia ni pamoja na kupata ajira kutokana na shughuli wanazofanya.


Ofisa miradi wa mfuko huo wa Kanda ya Kaskazini, Magreth Victor, alisema vijiji hivyo vinapatikana katika wilaya tano ambazo ni Muheza, Lushoto, Korogwe na Mkinga (Tanga) na Same (Kilimanjaro).

Alisema kila mwaka wamekuwa wakitoa Sh. milioni 49 kwa hifadhi hiyo, kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za uhifadhi, utunzaji wa misitu pamoja na utalii ikolojia ikiwemo kusafisha mipaka, kufanya doria na kuboresha vivutio vya watalii ikiwemo malazi.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Mabingwa wa salaam waliotesa RTD enzi hizo

Na Adam Fungamwango



Hawa ni baadhi ya watangazaji maarufu wa Redio Tanzania Dar es Salaam enzi hizo, baadhi yao ni Charles Hillary wa kwanza kushoto waliokaa, wa pili yake kulia ni Mikidadi Mahmooud, na Julius Nyaisanya wa kwanza kulia waliokaa.

DUNIA inakwenda kasi sana. Leo hii watu hawasalimiani kwa barua kama ilivyokuwa zamani. Siku hizi mitandao ya kijamii ya aina mbalimbali imechukua mkondo wake.

Siku hizi watu wanachati moja kwa moja, tena siyo kama wako Tanzania tu, hata mmoja akiwa Bongo na mwingine Marekani. Kitakachowatofautisha ni masaa tu ya sehemu.

Hivi sasa watu wanaweza kujiunga hata kikundi, wakaanza kujadili vitu mbalimbali kama mpira, siasa, muziki, na mambo mbalimbali ya maendeleo yao, sehemu wanayoishi, mikoa walikotoka na hata na nchi kwa ujumla.

Haikuwa hivyo zamani. Hata kwenye vyombo vya habari, hasa redio ambazo watu walikuwa wanasalimiana kupitia kadi za posta, maarufu kama postakadi.

Walikuwa wakizinunua posta na kuandika majina ya watu ambao wanataka kuwasalimia, wanaweka stempu na kuzitumbukiza kwenye kisanduku, kabla ya kupelekwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), kusomwa.

Postakadi hizo hizo zilikuwa zikisomwa mara nyingi kwenye vipindi maalum vya salamu kama vile 'Asubuhi Njema', 'Jambo', 'Mchana Mwema','Pole kwa Kazi', 'Jioni Njema' na vinginevyo.

Mtu yeyote tu anaweza kuchukua kadi na kuandika, akasalimia yeyote yule, lakini kulikuwa na watu ambao wao walikuwa kama vile ndiyo kazi yao ya kila siku.

Wao kazi yao kubwa ilikuwa ni kununua postakadi nyingi na kusalimia watu wengi na kuzituma. Halafu watu hao walikuwa na tabia ya kusalimiana wenyewe kwa wenyewe. Ni wale ambao huwa wanatuma mara kwa mara.

Hii ilisababisha watu hao kusikika karibuni kila kipindi cha salamu. Kama kadi yake haikusomwa basi atasalimiwa. Na kwa sababu hiyo mtu huyo anaweza akasikika kutwa nzima kwenye vipindi vya salamu.

Watu hawa wataitwa mabingwa wa salaam. Ilikuwa kila ukiamka utawasikia, wakisalimia na kusalimiwa. Na ukitaka kusalimia, ni lazima uwasalimie mabingwa hao.

Kwa sababu hiyo watu hao wakawa maarufu sana na kuzeoleka hata kwenye midomo na vichwa na wasikilizaji wa redio hiyo, wakati huo ikiwa moja tu.

Ikumbukwe kuwa kuna awamu mbili ya mabingwa wa salamu. Kuna ile iliyokuja baada ya ujio wa redio binafsi, ikiwemo Redio One, ambapo pamoja na kusomwa na postakadi, lakini ilikuwa ndiyo redio iliyoleta teknolojia ya mtu kupiga simu moja kwa moja na kusalimia laivu.

Awamu ya kwanza ya watuma salamu maarufu ya RTD, inaanza na mtuma salamu maarufu kabisa ambaye sidhani kama kuna mtu anayewafahamu watu hao watataja majina ya watu watatu bila kumtaja yeye. Huyu ni Wajadi Fundi wa Mahuta Shimoni, Newala.

Wengine ambao walikuwa maarufu miaka ya 1970 hadi miaka ya 1990, ni Issa Hasaan majeshi, Chivalavala M Chivalavala, Limonga Jastin Limonga, Dua Wajadi, Maalim Shaaban Uledi, Mungwangwa wa Mungwangwa, Ngariba Jongo na Kunguru Mwoga.

Wengine ni Damas Lusinde Nyingo, Nyembo Juma Nyembo, Uwesu Mbuzi, Ubwa Kombo, Nuru Mtoto, Boko Man, Hawa Kilongo, Tx Exaud Nko 'Surambili', Samwaja wa Samwaja, Kuwayawaya S Kuwayawaya, Juma Ramadhani Kamage, Ali Mbondei, Zamlata Jongo, Muungwana Zomboko, , Zacharia Ndemfoo, Thomas Mushi Kimboka, Thomas Myani, Kangoma H Kangomba, dereva Abdallah Mgeni, Abdallah Mpanjinji, Dk. Maulidi Tego na wengine wengi.


Hawa si tu kwamba walikuwa wanasalimiana, lakini kua taarifa kuwa walikuwa wanatembeleana na kusaidia. Bingwa wa salamu kutoka Tanga anaweza kwenda Kigoma kumtembelea mwenzake huko na kukaa huko hata wiki mbili kwa gharama na mwenyeji wake.

Baada ya enzi wa postakadi, ikaja sasa mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2000 ambapo mabingwa walikuwa wakipiga simu moja kwa moja na kutuma salamu.

Hapa sasa kikaja kizazi kingine cha mabingwa wa salamu ambao wengi bado watu wana kumbukumbu nao. na Hao

Hao ni John Zenze, Ndilana Mwambi, Jangala Kikongosi, Stephen Ishengoma, Bongo Experience, Juma Msurvivor, Teddy Big Mama, Manka Mushi, Papa Osama, Frank Malecela 'Mubosi', Manase Muhaha, Emma Kulaya, Jumanne Sebarua Tingisha, Chesco mzee wa Matunda, Manyota Top Manyota, Lawena Nsonda, Suzi Ngodoki na mtu mmoja mwenye mbwembwe Kung'ombe Chacha Werema Sukari Muhiri Obare. Mtangazaji akimwita Muhiri Obale ataitia hata dakika nzima kwa kuivuta herufi A 'Naaam.'

Hizi ndizo zilikuwa burudani za Mabingwa wa Salaam enzi za postakadi na baadaye simu za moja kwa moja za mezani. Kama kuna aliyesahaulika, msomaji unaruhusiwa kutuma meseji na kumtaja mwanasalamu ambaye hakuwekwa hapa.




Hizi ni Postikadi zilizokuwa zikitumiwa na wasikilizaji na watumasalamu maarufu enzi hizo.

# Wakuu wa majeshi SADC wakutana Goma

**GOMA,** DRC

MAPIGANO kati ya majeshi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na waasi wa M23 yanaweza kutokea wakati wowote baada ya wakuu wa majeshi kutoka nchi tano kukutana ghafla kujadili hali ilivyo mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Makamanda hao kutoka nchi za Afrika Kusini, Tanzania, Malawi, DRC na Burundi walikutana juzi katika mji wa Goma, mkoani Kivu Kaskazini kwa ajili ya majadiliano.

Kulingana na msemaji wa jeshi la DRC, mkuu wa jeshi la Afrika Kusini Jenerali Rudzani Maphwanya aliwasili Alhamisi mjini Goma na kujumuika na wakuu wengine kwa ajili ya mkutano huo.

Afrika Kusini, Malawi na Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa SADC ambazo zimepeleka wanajeshi wake na vifaa kusaidia vikosi vya serikali dhidi waasi wa kundi la M23.

Kanali Guillaume Ndike Kaiko, msemaji wa utawala wa kijeshi wa Mkoa wa Kivu Kaskazini, aliiambia BBC kwamba makamanda wa kijeshi wa nchi hizo walifika Goma Alhamisi lakini hakuzungumzia nini watajadili.

Shirika la habari la DRC lilisema kuwa kiongozi wa kwanza kuwasili Goma alikuwa mkuu wa jeshi la Tanzania Jenerali Jacob John Mkunda na ujumbe wa wa jeshi la Malawi.

Viongozi wengine waliohudhuria mkutano huo ni Jenerali Christian Tshiwewe, Kamanda Mkuu wa Jeshi la RDC, na Jenerali Prime Niyongabo ambaye ni Kamanda wa Jeshi la Burundi,

**BBC**

# UN yataka uchunguzi huru mauaji Gaza

**NEWYORK,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres , ametoa wito wa kufanyika uchunguzi huru kuhusu Wapalestina 117 waliouawa wakati wakisubiri msaada wa chakula Ukanda wa Gaza.

Katika tukio hilo lililotokea juzi, watu wengine 760 kujeruhiwa baada ya kikosi cha Israel kushambulia umati wa watu waliokusanyika na kulizunguka gari la msaada.

Guterres alilaani tukio hilo na kusema raia waliokata tamaa na wanaohitaji msaada wa haraka wanauawa bila hatia.

Hata hivyo, kundi la Hamas limeshutumu Israel kwa kuwafyatulia risasi raia, lakini serikali ya Israel ilisema watu wengi walikufa kwa mshtuko baada ya kufyatua risasi za ovyo.

Wakati huo huo, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema raia walilengwa na wanajeshi wa Israel.

Mkuu wa sera za kigeni wa EU, Josep Borell, alielezea tukio hilo kama mauaji yasiyokubalika kabisa.

Katika taarifa yake, Guterres aliandika kwenye mtandao wa kijamii kwamba analaani tukio lilotokea Alhamisi huko Gaza na kuua zaidi ya watu 100 au kujeruhiwa wakati wakitafuta msaada wa kuokoa maisha.

"Raia waliokata tamaa huko Gaza wanahitaji msaada wa haraka, ikiwa ni pamoja na wale wa kaskazini ambako Umoja wa Mataifa haujaweza kutoa msaada kwa zaidi ya wiki moja." alisisitiza Guterres.

Wizara ya afya ya Gaza inayoendeshwa na Hamas imelitaja tukio hilo kuwa ni mauaji ya kutisha.

Vyombo vya habari vya Palestina vilinukuu vyanzo mbalimbali vikisema kwamba wanajeshi wa Israel waliufyatulia risasi umati wa watu.

Chanzo kutoka jeshi la Israel kilisema wanajeshi walifyatua risasi wakiamini walikuwa hatarini.

Taarifa ya Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), ilisema makumi ya watu waliuawa kwa kukanyagwa na kupondwa na malori.

Mwandishi wa habari katika mji wa Gaza, aliliambia BBC kwamba vifaru vya Israel viliushambulia umati wa watu waliokuwa wamekwenda kuchukua mahitaji.

Video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha waliofariki katika Jiji la Gaza, wakiwa wamepakiwa kwenye malori ya misaada na mikokoteni ya kukokotwa na punda.

Tukio hilo lilitokea saa chache baada ya wizara ya afya ya Gaza kutangaza kuwa zaidi ya watu 30,000, wakiwemo watoto na wanawake 21,000.

**BBC**



Wapalestina wakibeba miili ya ndugu zao kwa kutumia mkokoteni wa punda baada ya tukio la watu zaidi ya 100 kuuawa wakati wakisubiri msaada wa chakula juzi. **PICHA: REUTERS**

# Kiongozi wa upinzani Chad Yaya Dillo auawa

**N'DJAMENA,** CHAD

KIONGOZI mkuu kambi ya upinzani nchini Chad, Yaya Dillo ameuawa katika makabiliano ya risasi na vikosi vya usalama.

Tukio hilo limetokea karibu na makao makuu ya chama chake katika mji mkuu wa nchi hiyo wa N'Djamena na kuibua hali ya wasiwasi.

Msemaji wa serikali, Abderaman Koulamallah, alisema kuwa Dillo aliuawa Jumatano kwenye makao makuu ya chama PSF, baada ya kukimbilia na kujifungia. Koulamallah ambaye pia ni Waziri wa Mawasiliano alisema Dillo alikataa kujisalimisha na aliwafyatulia risasi askari.

Mapema Alhamisi, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Chad, Oumar Mahamat Kedelaye, aliwataja watu waliouawa katika shambulizi hilo akiwemo Dillo bila kutoa maelezo zaidi kuhusu mazingira ya vifo hivyo.

Dillo alishutumiwa na serikali kwa kuongoza shambulizi dhidi ya ofisi ya idara ya usalama wa ndani usiku wa kuamkia Jumatano.

Hata hivyo, akizungumza na shirika la habari la Ufaransa (AFP), Dillo alikanusha kuhusika na shambulizi hilo na kuziita shutuma hizo za uwongo na zinachochewa kisiasa.

Alisema wakati mkasa huo unatoke, yeye hakuwepo katika eneo hilo. Juzi kulisikika milio ya risasi za kivita karibu na makao makuu ya chama hicho cha upinzani. Shirika la habari la Reuters liliripoti kuwa hali ya utulivu imerejea kwenye mji mkuu N'Djamena na wakazi wake walianza kwenda kazini.

Pia kulikuwa na idadi ndogo ya wanajeshi wanaoonekana mitaani, ingawa mtandao wa intaneti bado haujarudi.

Kabla ya tukio hilo, serikali ya Chad ilitangaza uchaguzi wa uraisi utafanyika Mei 6.

Rais wa mpito Mahamat Idriss Deby Itno na Dillo wote walitangaza nia yao ya kugombea nafasi hiyo. Katika tukio jingine, serikali ilisema mwanachama mmoja wa chama cha PSF, Ahmed Torabi alifanya jaribio la mauaji dhidi ya Rais wa Mahakama ya Juu, Samir Adam Annour.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Torabi aliuawa kwa kupigwa risasi siku ya Jumanne na mwili wake uliwekwa kwenye makao makuu ya idara hiyo.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**WINFRIDA GODWIN ELIAS** anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE028776** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **05/06/2018.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/23562/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERICK KISENDI BENJAMINI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1743/0027** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWAMALA SEKONDARI** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/27198/2024.**

## KUPOTEA KWA OFFER ORIGINAL YA KIWANJA

**SEIF HAMAD SALUM** anatangaza kupotea kwa **OFFER ORIGINAL YA KIWANJA PLOT NO.09, BLOCK E MIGANGA EAST - DODOMA CITY COUNCIL.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/5376/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1383/2024**
**In the matter of the Estate of the late CHARLES BENARD MWANIOTI of Msalato within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY RISHADA MUSSA KAZEWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18TH Day of MARCH, 2024

Date at Dodoma this 30th Day of JANUARY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AIZECK ELIUD NGWALE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T 154 BCT** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/2342/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Haptsam John Kilomba** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 968 AHT** aina ya **SANLG.** Kwa yeyote akatae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Haptsam kwa simu namba **0629766144.** Taarifa ya Polisi: **MGZ/RB/145/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JUDI HERENED KYANDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 416 ARN aina ya TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PK5E4A45945.** Engine namba **OK4AE4056909.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/NJO/NJO/388/2024.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DODOMA DISTRICTR REGISTRY)**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 994 OF 2024**
**In the matter of the estate of the late of**
**CALVIN AITAEL MAIMU**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by NARINDWA CALVIN MAIMU and HANSLEY CALVIN MAIMU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of March...................... 2024

Dated at Dodoma this 28th day of February................2024

DEPUTY REGISTRAR

**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3549 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**NEHEMIAH JOSEPH RAPHAEL**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JOSEPH NEHEMIAH JOSEPH AND NEEMA NEHEMIAH JOSEPH**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 03 rd Day of APRIL, 2024

Dated at Dodoma this 28TH Day of February, 2024.

PRINCIPAL/SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**E-MAIL: advertise@guardian.co.tz**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji wa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# HADITHI

# DAMU YA MARIAMU-2

Na Adam Fungamwango : (0716 350534)

Angeweza kuwa ana mshefa wa maana amempangia nyumba Masaki, Oysterbay, Mbezi Beach, na sehemu nyingine za ushuani.

Mwenyewe ameamua kuishi maisha ya kawaida tu. Amepanga nyumba ya vyumba viwili na sebule maeneo ya Tabata.

Amesumbuliwa sana na wanaume wenye hadhi na pesa, lakini wapi, harubuniki, hababaiki, kwani mwenyewe pamoja na umri wake mdogo tu wa miaka 25, ana maduka yake mawili ya vipodozi, Tabata na Buguruni, saluni ya kike Ilala na ya kiume Mtoni, vitega uchumi ambavyo vinamuingizia pesa zinazomtosha kabisa kuendesha maisha yake na kusaidia hata ndugu zake.

Ana mpenzi mmoja tu. Naye wala si tajiri, hana cheo wala umaarufu wowote. Ni fundi makenika. Watoto wa mjini wanasema fundi gereji. Kazi yake ni kutengeneza magari maeneo ya Buguruni Dar es Salaam.

Kwa sababu ni fundi mzuri wa kuaminika, pesa ya kula au kuvaa wala haikumpiga chenga.

Yeye ndiye alikuwa mkuu wa gereji hiyo. Mmiliki alimpa cheo hicho kwa sababu alimletea wateja wengi kutokana na umahiri wa kutengeneza magari.

Anaitwa Kamal. Huyu ndiye aliyekuwa akimiliki chuma hicho. Mrembo, tishio la jiji, Mariamu.

Walikutana kwa bahati mbaya tu kama ambavyo wapenzi wengi ambao walikuja kufunga ndoa walivyokutana. Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kusema alipanga kukutana na mpenzi wake, mke au mume aliyenaye. Huwa inatokea kwa bahati mbaya.

Ilikuwa ni Msamvu, Morogoro kituo kikuu cha mabasi. Kamal, ambaye alikuwa ametoka maeneo ya Kichangani kumsalimia dada yake alikuwa anarejea Dar es Salaam.

Alipofika kwenye kituo cha mabasi akachagua basi moja akapanda na kukaa eneo la dirishani.

Katika basi hilo abiria walikuwa wakikatishwa tiketi na kupanda bila kupewa namba ya siti. Unapoona panakufaa basi hapo hapo tu unakaa. Kwa sababu lilionekana halijai upesi, Kamal aliamua kuteremka chini kwanza na kushangaashangaa. Baada ya nusu saa hivi, alirejea tena ndani ya basi lile lile.




**Ofa ndiyo usiseme, kila kitu alikipata kwa urahisi sana, ingawa yeye hakuwa rahisi kama walivyodhani.**

Alipofika kwenye siti aliyokuwa amekaa awali, akashtuka. Sehemu ambayo alikuwa amekaa, ilikaliwa na mtu mwingine. Ni msichana mrembo ambaye uzuri wake haumithiliki.

Alisimama sekunde kadhaa akiushangaa urembo na mwanamke huyo ambaye hapo alikuwa akitazama asilimia ndogo tu kwenye sura yake na wala si mwili kwa sababu alikuwa amekaa.

Mdomo wake ni kama ulizuiwa kusema chochote alichotaka kusema. Sehemu ile alikuwa amekaa yeye. Sasa hivi imekaliwa na mwanamke mwingine. Akaiba macho kwa abiria wengine ambao wengi walimuona alikuwa amekaa pale kabla ya kutoka nje.

Wanaume wengi walionekana kumkodolea macho msichana yule, na Kamal alivyoingia wengi walijua udhaifu wa wanaume. Wakawa wanamuangalia kama atamtoa au la. Kwa uzuri na urembo alionao walijua kabisa kuwa jamaa atatepeta, atakaa upande mwingine ambao si wa dirishani.

Kamal alilitambua hilo. Alijua wengi wanataka kuona udhaifu wake. Alikaa pale, lakini sasa amekaa msichana huyo na kwa hali ya kawaida kwa wanaume wengi wangekubali yaishe. Asingemwambia lolote.

"Samahani dada." Akasema huku akisogeza hatua zake, lakini miguu ikionekana kuwa mizito.

"Bila samahani kaka." Akajibu kwa sauti ndogo, nyororo na ua utulivu, kiasi cha kumfanya Kamal kutaka kusitisha mpango wake.

Kwa sababu alikuwa na lengo maalum, akaona bora aendelee tu. Wakati huo abiria wengi alikuwa wanataka kuona nini kinaendelea, hivyo kila mmoja jicho na sikio lake lilikuwa huko.

Tayari abiria wawili wapya waliingia na kulifanya basi kufikisha abiria 60 na likaanza kujiandaa kuondoka.

"Hapo ulipokaa ni kwangu. Nilikuwa nimekaa mimi awali. Nilishuka tu kwenda kupunga upepo nje."

"Okay, sawa kaka nimekuelewa. Ila naomba mimi nikae huku dirishani, wewe upande huu. Siti si hii hii moja bwana!"

"Kwa nini?" Akauliza Kamal akionekana hajakubaliana na hilo.

"Samahani, ni kweli kuna kaka mmoja akaniambia hapo kuna mtu, lakini mimi naomba nikae huku dirishani kwa sababu huwa nina kichefuchefu."

"Okay, hata mimi nina kichefuchefu, ndiyo maana nimechagua siti ya dirishani. Kwanini na wewe hukuchagua siti ya dirishani?"

"Nilikuta zimejaa kaka yangu."

"Basi bahati mbaya sana. Naomba tu nikae kwenye nafasi yangu." Akasema huku akiwa hamuangalii usoni.

Kila mmoja ndani ya basi hakutegemea lililotokea. Walichofikiri sicho. Walidhani Kamal atalainika na kukubali kukaa upande mwingine kutokana na urembo alionao binti yule.

Walijiuliza ni mwanaume wa aina gani? Mwanaume asiyeonyesha upendo wala dalili za kujali au kumsaidia mrembo yule kwa sababu zozote zile.

Hata Mariamu mwenyewe alishangaa. Hajawahi kukutana na mwanaume wa aina ile kwenye maisha yake. Mwanaume mkavu kama samaki aliyeanikwa juani.

Anachofahamu yeye ni kwamba tangu aanze kuitwa mkubwa alipofikisha umri wa miaka 17 tu, wanaume wamekuwa wakijilegeza, kujigonga, kujipendekeza na kumpa misaada yoyote hata ambayo haihitaji.

Ofa ndiyo usiseme, kila kitu alikipata kwa urahisi sana, ingawa yeye hakuwa rahisi kama walivyodhani.

Leo kwa mara ya kwanza na hakumbuki lini, amekutana na mwanaume ambaye haangalii uzuri, urembo wala haiba yake ya kike.

Alichodhani kuwa yoyote ambaye alikuwa amekaa siti ya dirishani, kama ni mwanaume, atakapofika na kumtazama tu, basi asingeweza kufanya kitu chochote. Angemkubalia kukaa dirishani bila masharti yoyote. Leo haikuwa hivyo.

"Ni mwanaume wa wapi huyu?" Mariamu akajiuliza.

"Dada nadhani umesikia nilichokuambia." Akarudia tena Kamal kwa sauti ya upole na unyeyekevu, japo alichokuwa akikitaka hakikuwa cha unyeyekevu.

Mariamu sasa akaamua tu kukubali yaishe. "Nakupisha kaka yangu." Akasema kwa sauti ya hasira kidogo iliyochanganyikana na aibu. Kwa mara ya kwanza ndipo alipogundua kuwa si kwa asilimia zote uzuri au urembo alionao unaweza kumpa au kumsaidia kila kitu. Akakumbuka usia wa marehemu mama yake aliowahi kumwambia.

"Mwanangu usibabaishwe na uzuri ulionao. Usiutumie uzuri wako kutaka kukurahisishia mambo yako. Akili, juhudi na maarifa uliyonayo ndiyo ikupatie namna ya kuishi, siyo uzuri.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# KMKM YABANWA LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Zanzibar KMKM SC wameendelea kubanwa mbavu kwenye michezo yao ya Ligi Kuu visiwani hapa baada ya juzi kuambulia suluhu kwenye mchezo wao dhidi ya 'vibonde' Ngome FC.

Mchezo huo ambao ulikuwa wa mzunguko wa 20, umkechezwa juzi kwenye uwanja wa Mau A mjini Unguja.

Kama KMKM SC ingefanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo huo, ingejihakikishia kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi kwa kuwa ingefikisha pointi 41 lakini matokeo waliyoyapata yameifanya kuendelea kubaki katika nafasi ya pili ikiwa na pointi 39 wakati Ngome FC wakipanda kwa nafasi moja kutoka mkiani hadi nafasi ya 15 baada ya kufikisha pointi 16.

Akizungumza na Nipashe Kocha Mkuu KMKM, Ame Msimu, alikiri michezo yote iliyosalia mpaka kumaliza msimu itakuwa migumu kutokana na kukaribiana alama katika msimamo wa ligi.

Alisema tangu hapo awali walijua mchezo wao dhidi ya Ngome FC utakuwa wa kuhitaji alama kwa kila mmoja wao hivyo licha ya kucheza kwa tahadhari na umakini hawakuwa na bahati kupata alama tatu.

**Alisema ni kawaida ukicheza na timu ambayo ipo chini katika msimamo wa ligi mchezo huo huwa mgumu kwakuwa na wao wanahitaji alama za kujinasua kutoka chini ili kutengeneza mazingira ya kubaki Ligi Kuu.**

"Wachezaji walicheza vizuri na kufuata mipango yote katika mchezo huu, lakini kulichokosekana ni umakini wa kutumia nafasi tulizotegeneza, tulipoteza mipira mingi wakati tunashambulia lango la wapinzani wetu, ila nafikiri hali hii imetokana na presha ya mchezo wenyewe"Alisema.

Aidha alisema bado anaimani anaweza kutetea taji lake la Ligi Kuu ya Zanzibar licha ya kuwepo kwa vizingiti vingi vinavyotokana na ugumu wa Ligi na timu zilizopo katika mbio za taji hilo.

"Bado tunayo nafasi ya kurekebisha makosa yetu, tumebakiwa na michezo kumi, hivyo michezo hii tutahakikisha tunajipanga vizuri ili tusifanye makosa".Alisema.

Hata hivyo Ligi kuu ya Zanaibar ilipaswa kuendelea leo Machi 2, lakini imesimama kufuatia msiba wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi aliyefariki juzi.

Michezo ya Ligi zote itaendelea baada ya siku saba za maombolezo kama ilivyotangwaza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan.

Taarifa ya kusimama kwa shughuli zote za michezo na burudani Zanzibar imetolewa na Ofisi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ).



Vijana wakiwania mpira walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ligi kikapu Dar kuanza leo

**Na Oliver Albert**

LIGI ya Mpira wa Kikapu mkoa wa Dar es Salaam (BDL) msimu huu inaanza leo kwa mabingwa watetezi Dar City kupambana na JKT kwenye uwanja wa Don Bosco Upanga .

Ligi hiyo inashirikisha timu 16 kwa wanaume na 16 kwa wanawake huku kwa upande wa wanawake leo mabingwa watetezi Vijana Queens wataonyeshana kazi na City Queens.

Kocha wa Dar City, Mohammed Mbwana alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaanza kwa ushindi katika ligi hiyo.

"Tuko vizuri tayari kwa mchezo. Tunajua utakuwa mchezo mgumu kutokana na aina ya wapinzani tunaokutana nao lakini tumejipanga vizuri kuwakabili," alisema Mbwana.

Kwa upande wake, Kocha wa JKT, Christian Jacob 'Webber' alisema jambo kubwa wanalotaka kuanza nalo ni kushinda mechi hiyo.

"Ukianza ligi kwa ushindi ni jambo zuri na ndicho ambacho sisi tumepanga kufanya. Wapinzani wetu ni moja ya timu nzuri hivyo tukutane uwanjani, " alisema.

Mchezo huo wa leo ambao utaanza saa 2 usiku ambao utakuwa wa ufunguzi wa ligi hiyo, unaleta kumbukumbu ya fainali ya msimu uliopita ambayo ilizikutanisha timu hizo na Dar City kuibuka mabingwa.

Timu hizo ndizo zilikutana fainali ya ligi hiyo mwaka jana na Dar City kushinda mechi ya mwisho kwa pointi 69-63 na kutwaa ubingwa.

Ushindi wa mechi tatu kati ya nne za fainali ndizo ziliamua ubingwa wa Dar City kwani ilishinda mechi tatu kwa pointi 75-61, 75-56 na 69-63 wakati JKT walishinda mechi moja tu kwa pointi 68-55.

Mechi nyingine za ufunguzi ligi hiyo leo kwa wanaume zitakuwa kati ya DB Oratory watakaocheza na Srelio wakati kwa upande wa wanawake kutakuwa na mechi nyingine kati ya Jeshi Stars dhidi ya Twalipo Queens na Mgulani Stars itaikabili JKT Stars.

## Singida FG yaipania Mtibwa

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Singida Fountain Gate FC, imesema imejipanga vizuri kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya Mtibwa Sugar na wanachotaka ni pointi tatu pekee.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa klabu hiyo, Hussein Masanza, alisema kuwa licha ya Mtibwa kuwa katika nafasi ya chini kwenye msimamo bado wameipangia mikakati kuhakikisha wanapata ushindi mbele yao.

"Tunataka kurejea kwenye kasi yetu, kwenye utaratibu wetu wa kushinda mechi za ligi, Mtibwa tuna waheshimu lakini ukweli hatutawaonea huruma, tunazitaka pointi tatu," alisema Masanza na kuongeza,

"Bado tuna nafasi ya kufanya vizuri katika mchezo wetu huo lengo ni kupata pointi tatu ili tuwape burudani mashabiki wetu msimu huu, alisema.

Alisema kikosi chao kipo imara na kila mchezaji anautaka mchezo huo ili kurejesha morali ya timu kuelekea kwenye michezo mingine ya ligi kuu.

"Tunaomba mashabiki wetu waje kwa wingi kesho (leo) washuhudie burudani itakayoonyeshwa na wachezaji wao tunaamini wao wana mchango mkubwa kwetu, uwepo wao utaongeza hamasa kubwa kwa wachezaji wetu.

## Mabondia watakiwa kujituma kufikia malengo

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA hapa nchini wametakiwa kujituma zaidi na kutokata tamaa ili wafikie mafanikio katika mchezo huo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Kocha wa bondia Mada Maugo, Mmarekani Seko Tongola , ambaye amesema kwenye kila mafanikio kunahitajika uvumilivu kujituma na nidhamu.

"Ninawashauri mabondia wote hapa nchini wajitume ili wawe na mafanikio kama walivyo wenzao wa nje ya nchi, alisema Tongola ambaye ni Mtanzania aliyechukua uraia wa Marekani

Alisema, wapo baadhi ya mabondia wamekuwa wakipigana mara kwa mara bila ya kujiwekea malengo na kujikuta wakipotea kwenye ngumi bila kuwa na kitu cha kujivunia kwa maisha ya baadae.

Aliongeza kuwa licha ya kuwa anaishi nchini Marekani yupo tayari kufundisha yeyote atakayehitaji msaada wake kwani lengo lake ni kuona vijana wengi wanafanikiwa.

"Japokuwa ninafundisha mabondia kutoka Mataifa mbali mbali pale Marekani, ninathamini nchi yangu mama ndio maana nimelazimika kuja kumsimamia Mada Maugo kuelekea kwenye pambano lake atakalocheza mwezi Aprili mwaka huu dhidi ya Karim Mandonga nipo tayari kumsaidia anayehitaji msaada wangu, alisema.

Kocha huyo alisema ameshauri bondia yeyote asilewe sifa mara tu anaposhinda kwenye pambano lake bali apigane kwa malengo ambayo yatasaidia vizazi vijavyo.

Alisema amesaidia mabondia wengi ambao walimsikiliza na kufuata kile alichowaelekeza hatimaye wamefanikiwa na ndoto zao kutimia.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVER KUMUUZA DIAZ

LIVERPOOL itakuwa tayari kupokea ofa ya kumuuza mshambuliaji wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27 msimu wa joto ikiwa mashambuliaji wa Misri Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, atakubali mkataba mpya. (***Sun***)

### SALAH PAUNI MIL 100

LIVERPOOL itataka ada ya zaidi ya pauni milioni 100 ili kumuuza Salah kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia msimu msimu huu kwa hiyo wanaamini watakuwa na fedha zinazohitajika za kujaza nafasi yake. (***Football Insider***)

### SPURS YAKOMAA NA GALLAGHER

KLABU ya Tottenham Hotspur inaendelea kufuatilia hali ya kiungo wa England, Conor Gallagher huko Chelsea na wako tayari kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 msimu wa joto. (***Daily Mail***)

### JORGINHO MKATABA MPYA

ARSENAL inajiandaa kuanza mazungumzo na kiungo wa kati wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 32, kuhusu mkataba mpya. (***Evening Standard)***

### ZEBRI ANUKIA MAN UNITED

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi ni mshindani mkubwa katika mbio za kuwania nafasi ya kuwa mkukufunzi wa ajaye wa Manchester United. (***Football Insider***)

### GETAFE KUMBAKISHA MASON

KLABU ya Getafe iko tayari kuanzisha mazungumzo na Manchester United kuhusu kuongeza muda wa kubakia kwa Mason Greenwood katika klabu hiyo, kwa kuafikiana mkataba mwingine wa mkopo na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22 au uhamisho wa kudumu. (***Time***)

### CANCELO, FELIX KUBAKI

BARCELONA inataka kuwabakisha wachezaji wa Ureno wanocheza kwa mkopo, Joao Cancelo na Joao Felix msimu ujao. Wako tayari kuilipa Manchester City kati ya euro milioni 15 na 20 kumpata Cancelo mwenye umri wa miaka 29 na kumchukua mshambuliaji Felix mwenye umri wa miaka 24 kwa mkataba mwingine wa mkopo kutoka Atletico Madrid. (***Sport***)

### RAMSDALE AWANIWA CHELSEA

CHELSEA inaweza kumnunua mlinda mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, wakati wa usajili wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### CHALOBAH ASIKITISHWA

MLINZI wa England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24 anataka kubakia Chelsea na amesikitishwa na klabu hiyo kufikiria kumuuza msimu huu wa joto. (***Teamtalk)***

### DIER UHAMISHO WA KUDUMU

MLINZI wa England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 30, ametimiza masharti ya kimkataba yanayohitajika kubadilisha uhamisho wake wa mkopo wa Bayern Munich kutoka Tottenham Hotspur kuwa uhamisho wa kudumu mwishoni mwa msimu. (***Athletic***)

### BELLANOVA AFUATILIWA

MANCHESTER United na Aston Villa zimetuma maskauti kumfuatilia beki wa Torino, Mtaliano Raoul Bellanova mwenye umri wa miaka 23. (***Tuttosport)***

## DONDOO Z OKA MAGAZET LAYA



# RASHFORD AWAJIA JUU WANAOMKOSOA

**MANCHESTER,** England

**●●● Nyota huyo anaamini amekuwa akitendewa ndivyo sivyo na vyombo vya habari, lakini ameweka wazi kuwa...**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford amewajibu wakosoaji wake wanaohoji kujitolea kwake katika klabu hiyo ya Ligi Kuu England baada ya kusimamishwa kwa utovu wa nidhamu msimu huu na kocha, Erik ten Hag.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 26 alikosa mchezo wa ushindi wa 4-2 wa United wa Kombe la FA raundi ya nne dhidi ya Newport County mwezi huu, siku chache baada ya kuonekana katika klabu ya usiku huko Belfast.

**Rashford, ambaye alifunga mabao 30 msimu uliopita, ameifungia United mabao matano tu msimu huu, na anaamini amekuwa akitendewa ndivyo sivyo na vyombo vya habari.**

"Ninapokosea, nitakuwa wa kwanza kuinua mkono wangu na kusema kwamba nahitaji kufanya vizuri zaidi. Lakini ikiwa utatilia shaka kujitolea kwangu kwa Man United, hapo ndipo ninapolazimika kuzungumza," alisema fowadi huyo akinukuliwa na vyombo vya habari vya Ulaya.

"Nilikua hapa. Nimeichezea klabu hii tangu nikiwa mvulana. Familia yangu ilikataa fedha za kubadilisha maisha nilipokuwa mtoto ili nivae beji hii.

"Iwapo utaanza kutilia shaka kujitolea kwangu kwa klabu hii na mapenzi yangu kwa soka basi nakuomba tu uwe na ubinadamu zaidi."

Rashford alipata sifa wakati wa janga la COVID-19 alipozindua kampeni ya kusaidia chakula kwa watoto ambayo ilisababisha Serikali ya England kutoa sapoti yake kwa kampeni hiyo.

Mchezaji bora wa mwaka wa United msimu uliopita anaamini kazi yake nje ya uwanja pia imesababisha kukosolewa.

"Nilikuwa nikijaribu tu kutumia sauti yangu kuhakikisha kwamba watoto hawakuwa na njaa kwa sababu najua hasa jinsi mambo yalivyo," alisema.

"Kwa sababu fulani, hiyo ilionekana kuwapotosha watu fulani.

"Inaonekana kama wamekuwa wakiningojea kuwa na wakati wa kibinadamu ili waweze kunyoosha kidole na kusema, 'Unaona? Ona yeye ni nani hasa?'

United wana msimu mbaya, wakiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pointi nane nyuma ya Aston Villa iliyo nafasi ya nne.

"Ninakuahidi, ulimwengu haujaona wachezaji bora wa kikosi hiki cha United na wachezaji hawa.

Tunataka kurejea kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya," Rashford alisema.

"Lazima tuendelee kufanya kazi, na hiyo inaanza na mimi."

# ROONEY AFICHUA NIA YA KUWA KOCHA MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

WAYNE Rooney amefichua kuwa kocha wa Manchester United ni "kazi ya ndoto yangu" licha ya maisha yake ya ukocha kukumbana na kikwazo baada ya kutimuliwa haraka kutoka Birmingham City.

Rooney ndiye mfungaji aliyeweka rekodi ya mabao 253 katika kipindi cha miaka 13 ya uchezaji wake pale Old Trafford.

Kisha alianza hatua inayofuata ya safari yake ya soka kwa kuwa kocha mchezaji pale Derby County, kabla ya kurejea klabu yake ya zamani ya D.C. United na kisha kuwa na siku 83 za kuinoa Birmingham.

Nahodha huyo wa zamani wa England alifikisha umri wa miaka 38 Oktoba mwaka jana na bado ana uwezekano wa miongo kadhaa ya kufundisha na usimamizi mbele yake.

Kwa hiyo, anabakia na matumaini ya kupata kazi nyingine na hatimaye kufanya kazi yake hadi kileleni mwa mchezo kwa wakati ufaao.

"Kwa hakika nataka kurejea kwenye uongozi. Lengo ni kusimamia katika Ligi ya England, Manchester United au Everton ndio kazi ya ndoto yangu, lakini ni mchakato," alisema Rooney akinukuliwa na BBC One.

"Katika miaka kumi ijayo, natumaini naweza kuwa na nafasi ya kuchukua moja ya kazi bora.

"Ilikuwa ni kikwazo kilichotokea Birmingham, lakini mimi ni mpiganaji. Unajua kama kocha sehemu ya kazi inafukuzwa na kuwa na vikwazo na ni jinsi unavyorudi nyuma. Labda muda haukuwa sawa nilipoingia nikiwa Birmingham, mashabiki hawakunikubali kuanzia siku ya kwanza."

# Sterling hana mpango wa kujiunga Al Hilal

**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea, Raheem Sterling haonekani kupendezwa na tetesi za uhamisho wa kwenda Ligi Kuu ya Saudi Arabia, huku mabingwa Al Hilal wakionesha nia ya kumtaka.



Watu wengi wenye majina makubwa barani Ulaya bado wanahusishwa na uhamisho wa kwenda kwenye taifa hilo tajiri la Ghuba, lililochochewa na mabadiliko ya Cristiano Ronaldo kwenda Al Nassr mwishoni mwa 2022.

Lakini Sterling anaonekana kusita, kwani mwandishi nguli wa michezo, Fabrizio Romano ameripoti kwamba kambi yake "haijawahi kushiriki au kujadili" uwezekano wa uhamisho wa kwenda Al Hilal.

Fabrizio pia aliwanukuu wawakilishi wakisema: "Raheem amejitolea kama zamani katika mradi wa Chelsea."

Baada ya kukaa kwa miaka 12 kaskazini magharibi mwa England akiwa na Liverpool na Manchester City, nyota huyo wa zamani wa akademi ya QPR, Sterling alirejea London mwaka 2022 kujiunga na Chelsea kwa ada ya pauni milioni 50.

Alikuwa ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu England akiwa na City, na hata alifunga mabao 31 katika mashindano yote msimu wa 2019/20 pekee.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 hajawa katika kiwango bora akiwa na kikosi cha Chelsea katika kipindi cha hivi karibuni kutokana na mabadiliko makubwa ya wachezaji.

Sterling ameanza mechi nyingi za Ligi Kuu kwa Chelsea msimu huu, lakini amefunga mara moja pekee kwenye mashindano yote tangu mwishoni mwa Novemba, licha ya bao muhimu katika sare ya 1-1 dhidi ya klabu yake ya zamani.

Kushuka kwa kiwango na kuongezeka kwa umuhimu wa wachezaji kama Bukayo Saka na Phil Foden pia kumesababisha nafasi yake kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England kuwa hatarini, na hajaitwa tangu Kombe la Dunia la 2022.

Licha ya Sterling kutokuwa na mpamgo huo, lakini klabu za Ligi Kuu Saudia hazitapunguza matarajio yao wakati dirisha la usajili la majira ya joto linapokaribia.

## Bosi LaLiga ataka Greenwood abaki

**MADRID,** Hispania

RAIS Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas anataka fowadi wa Manchester United, Mason Greenwood abaki nchini humo mara baada ya mkopo wake wa msimu mzima katika klabu ya Getafe utakapomalizika.

Greenwood mwenye umri wa miaka 22, alijiunga na kikosi cha Madrid akitokea United Septemba mwakam jana baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa England kuachana na klabu yake ya zamani kufuatia uchunguzi wa uhalifu kuhusu uwezekano wa kujaribu kubaka.

Mashtaka dhidi ya Greenwood yalitupiliwa mbali, lakini aliihama klabu hiyo kufuatia uchunguzi wa ndani.

"Yeye (Greenwood) anaendelea vizuri kama mchezaji na ninatumani ataendelea kubakia katika soka la Hispania," alisema Tebas akiwaambia waandishi wa habari mjini London.

"Hiyo ni nzuri kwetu."

Greenwood, ambaye amefunga mabao matano na kutengeneza mengine matano katika mechi 25 alizochezea Getafe, ana mkataba na United hadi Juni 2025.

Mmiliki mwenza mpya wa United, Sir Jim Ratcliffe hivi karibuni aliulizwa kuhusu Greenwood na kusema: "Tunahitaji kuangalia ukweli, kuhukumu kwa haki na kuzingatia maadili ya klabu ni nini. Kisha tunatoka katika hilo na uamuzi. Kwa sasa haifai kwangu kutoa maoni juu ya Mason Greenwood."

Tebas, mwanasheria kitaaluma, alisema hana nia ya kumhukumu Greenwood kwa sababu "hajahukumiwa" na mahakama.

"Unapaswa kuheshimu mchakato wa kisheria," alisema Tebas.

"Watu wanaweza kuwa wanamhukumu kwenye vyombo vya habari, lakini unapaswa kuheshimu uamuzi wa kisheria. Hakuna kitu kingine cha kuzungumza juu yake. Hakuhukumiwa na maana yake hakupatikana na hatia."



HABARI MICHEZO

## Simba, Jwaneng Galaxy mechi..

INATOKA UK 24

nakuja kutafuta pointi tatu, nao wana nafasi ya kusonga mbele, lazima tuwe makini licha ya kucheza nyumbani, haya yote tumeambiana kwenye uwanja wa mazoezi," alisema Benchikha.

Rekodi zinaonyesha kabla ya msimu ambao Jwaneng waliwatibulia kutinga hatua ya makundi, msimu wa 2018/19 Simba ilikutana na mazingira kama ya msimu huu katika mechi ya mwisho ya makundi dhidi ya AS Vita ambapo ilikuwa ikihitaji ushindi tu kutinga robo fainali na ikafanya hivyo kwa kuifunga AS Vita mechi ya mwisho mabao 2-1.

Msimu uliofuata katika mazingira kama hayo Simba iliichapa tena AS Vita mabao 4-1 katika mechi ambayo ilikuwa inahitaji ushindi kungia makundi.

Msimu wa 2021/2022 Simba ilikutana tena na mazingira kama hayo kwenye kombe la Shirikisho Afrika ikapata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Gendarmerie na kutinga robo fainali ikarudia tena msimu wa 2022/2023 kwa kuifunga Horoya ya Guinea mabao 7-0 mechi ya mwisho na kutinga hatua ya robo fainali.

Kocha wa Jwaneng Galaxy, Morena Ramoreboli kuelekea mchezo wa leo amesema walikuwa hapa tanzania miaka mitatu iliyopita na wakaondoka na pointi tatu hivyo wanataka kurudia walichokifanya.

## Aziz Ki hatari nje ya boksi,

INATOKA UK 24

Wachezaji wengine ambao wana mabao mengi waliyoyafunga wakiwa ndani ya eneo la hatari ni Jean Baleke ambaye alikuwa akichezea Simba na sasa ameondoka kwenye kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo akiwa amefunga mabao saba ndani ya boksi kwenye mabao nane aliyofunga kabla ya kuondoka Simba.

Baleke anaungana na Prince Dube wa Azam na Maxi Nzengeli wa Yanga wenye idadi hiyo ya magoli ya ndani ya boksi.

Kiungo wa Simba Saido Ntibazonkiza, bado ameendelea kuwaburuza wenzake katika mabao ya penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Kiungo huyo raia wa Burundi ana mabao manne aliyoyafunga kwa mikwaju ya penalti huku takwimu za dawati la gazeti hili zikionyesha hakuna hata mchezaji mmoja wa Ligi Kuu aliyefunga zaidi ya bao moja kwa njia hiyo.

Takwimu za Nipashe zinaonyesha wachezaji 13 wa Ligi Kuu wamefunga penalti moja moja kila mmoja, ambao ni Febrice Ngoy na Derick Mulokozi wote wa Namungo, Pacome Zouzoua na Stephane Aziz Ki wa Yanga, Jean Baleke wa Simba, Prince Dube na Feisal Salum wa Azam FC, Obrey Chirwa wa Kagera Sugar, Daniel Lyanga JKT Tanzania, Ibrahim Ajibu na Lucas Kikoti wote wa Coastal Union, Erick Okutu wa Tabora United na Jumanne El Fadhil wa Prisons.

# COASTAL, PRISONS FC ZAFUKUZA MWIZI KIMYA KIMYA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

INGAWA zimekuwa hazizungumzwi sana, timu za Coastal Union na Prisons zimeonekana kuwa tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, zikipata matokeo mazuri na kupanda juu ya msimamo kwa kasi kiasi cha kuwa tishio.

Timu zote mbili zilikuwa na matokeo mabovu katika mechi za mzunguko wa kwanza, lakini zikafanya mabadiliko makubwa kwenye mabenchi yao ya ufundi mwishoni mwa mzunguko huo na sasa mabadiliko hayo yanaonekana kuwalipa.

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata wiki hii dhidi ya Mtibwa Sugar umeifanya timu hiyo kufikisha pointi 26 na kupanda mpaka nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi.

Mara ya mwisho kupoteza mechi kwa Coastal Union ilikuwa Novemba 27 mwaka jana, ilipokubali kipigo cha magoli 2-1 kutoka kwa Singida Fountain Gate, lakini baada ya hapo imecheza mechi sita, ikishinda tano na kutoa sare mechi moja.

Mechi ambazo imecheza baada ya hapo ni dhidi ya Geita Gold, ikishinda mabao 3-1, ikaichapa Kagera Sugar bao 1-0, ikapata ushindi kama huo dhidi ya JKT Tanzania, Dodoma Jiji na Mtibwa Sugar na suluhu ya bila kufungana dhidi ya KMC.

Prisons inashika nafasi ya tano, nayo imeonekana kufanya vizuri kimya kimya, ikifikisha pointi 24 kwa michezo 18 ambayo imecheza mpaka sasa.

Ushindi wa mabao 2-1 ilioupata dhidi ya Tabora United, umeifanya kufikisha pointi hizo na kuwa katika nafasi za juu ambazo haijawahi kufika kwa misimu mingi sasa.

Katika mechi 10 za mwisho ilizocheza, imepoteza mechi tatu tu, ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar na Yanga, pamoja na bao 1-0 dhidi ya Coastal Union.

Katike mechi hizo imeshinda mechi tano, kwa kuzifunga Dodoma Jiji na Namungo bao 1-0 kila mmoja, ikapata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa, ikaichapa Singida Fountain Gate mabao 3-1, Tabora United mabao 2-1, huku ikitoa sare mbili, dhidi ya Ihefu na Azam kwa kufungana bao 1-1.




Kocha wa Simba, Abdelhak Benchikha (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mchezo wao wa leo wa Klabu Bingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy, kulia ni mchezaji wa Simba, Omari Jobe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzanite yaingia kambini kujiandaa 'All Africa Games'

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20 'Tanzanite' imeingia kambini jana na tayari imeanza mazoezi kujiandaa na mashindano ya 'All Africa Games' yatakayofanyika Accra, Ghana kuanzia Machi 8 hadi 23, 2024.

Tanzanite chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime, imepangwa kundi A ikiwa na timu za Ghana , Uganda na Ethiopia.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo alisema timu ya Tanzanite imeingia kambini kujiandaa na michuano hiyo na tayari wameanza mazoezi.

Alisema kulingana na maandalizi yanayoendelea kufanyika, TFF wana matarajio makubwa timu hiyo kufanya vizuri katika kundi lao.

"Tunaimani kubwa na kikosi cha U-20 kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa kuwa baadhi ya wachezaji waliokuwepo kwenye timu ya Twiga Stars ndio hao wanaunda kikosi cha Tanzanite, nina uhakika uzoefu waliupata wakiwa na Twiga Stars utaisaidia timu," alisema Ndimbo.

Alisema, TFF itaendelea kua karibu na timu hiyo na timu nyingine za taifa hili ziweze kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali.

Kikosi cha Tanzanite kinaundwa na golikipa Husna Mtunda (Yanga) na Washambuliaji Winifrida Gerald, Christer Bahera, Jamila Rajabu, Joyce Lema (JKT Queens), Violeth Nicholaus na Asha Mnuka (Simba), Hasnat Ubamba (Fountain Gate Princess)

Wachezaji wengine ni Zulfa Makauo, Lydia Maximilian, Jackline Shija na Alia Fikiri (JKT Queens), Mariam Shaban, Ester Maseke na Jamila Selestine (Bunda Queens).

Wengine ni Sarah Joel (Fountain Gate Princess), Koku Kipanga na Zainabu Mohammed (Simba Queens), Sabina Alex (Geita Gold Queens ), Neema Paul na Asha Omari (Yanga).

Michezo
Nipashe
Jumamosi Machi 2, 2024



Rashford awajia juu wanaomkosoa UK. 21



# SIMBA, JWANENG GALAXY MECHI YA MAAMUZI CAF

Na Saada Akida

## ●●● Benchikha asema kazi imebaki kwa wachezaji, ataka wamalize mechi mapema...

MBALI ya kuwa mechi ya leo Simba dhidi ya Jwaneng Galaxy ni ya kulipiza kisasi kwa upande wa wekundu hao wa msimbazi baada ya kuondoshwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya kwanza dhidi ya Wabotswana hao mwaka 2021, mechi hii itatoa maamuzi ya nani atatinga hatua ya robo fainali msimu huu na kuungana na Asec Mimosas ambao tayari wamekata tiketi ya kutinga hatua hiyo.

Simba inaumana na Jwaneng Galaxy kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 1:00 jioni kusaka ushindi tu kuweza kutinga hatua hiyo bila kuangalia matokeo ya mchezo kati ya Wyadad Casablanca dhidi ya Asec Mimosas ambao nao wanacheza leo.

**Timu tatu, Simba, Wydad na Jwaneng zote zina nafasi ya kutinga hatua hiyo lakini zitapaswa kuangalia matokeo ya kila timu kwenye mechi za leo za mwisho hatua ya makundi.**

Endapo Simba itashinda dhidi ya Jwaneng Galax, moja kwa moja itakuwa imefuzu robo fainali bila kuangalia matokeo ya Wydad Casablanca, lakini endapo itapoteza itatoa nafasi kwa Wamorocco hao kufuzu kama watapata ushindi dhidi ya Asec.

Ili Jwaneng Galaxy iweze kufuzu hatua hiyo itapaswa kuifunga Simba na kuiombea Wydad Casablanca ifungwe na Asec.

Kocha wa Simba, Abdelhak Benchikha akizungumza jana kuelekea mchezo wa leo, amesema ni mchezo muhimu kwao kuwapa furaha mashabiki wao na Watanzania kwa ujuma.

Alisema wamejiandaa vizuri kwenye uwanja wa mazoezi na wachezaji wake wanafahamu umuhimu wa mechi hiyo.

"Kazi imebaki kwa wachezaji kutekeleza yale tuliyoyafanyia mazoezi, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata ushindi, hatuangalii mechi za timu nyingine, sisi tunapambana kwenye mchezo wetu kupata ushindi," alisema Benchikha.

Alisema katika historia ya hivi karibuni Simba imekuwa na rekodi nzuri ya kupata ushindi katika mechi kama hizi ambazo huwa inatakiwa ipate ushindi iweze kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini wanahitaji kuwa makini kuendeleza rekodi hiyo.

"Wapinzani wetu nao wa-

INAENDELEA UK 23

## Aziz Ki hatari nje ya boksi, Fei Toto ndani

Na Adam Fungamwango

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akiongoza kwa kufunga mabao akiwa nje ya eneo la hatari, kiungo wa Azam FC, Feisal Salum ameonekana kuwa hatari kwa kufanya hivyo akiwa ndani ya boksi.

Aziz Ki, ambaye anaongoza kwa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na mabao 10, anaongoza kwa kufunga mabao akiwa nje ya eneo la hatari ambapo mpaka sasa ana mabao manne akiyafunga nje ya boksi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Burkina Faso anafuatiwa na kiungo wa Ihefu FC raia wa Togo, Marouf Tchakei mwenye mabao matatu, huku Clatous Chama, Mzambia anayeichezea Simba akishika nafasi ya tatu kwa kufunga mabao nje ya boksi, akifanya hivyo mara mbili, sambamba na wachezaji Velentino Mashaka na Tariq Seif, wote wa Geita Gold.

Kiungo mshambuliaji Mtanzania, Fei Toto yeye anaongoza kwa kupachika mabao akiwa ndani ya boksi.

Amepachika mabao manane akiwa ndani ya eneo la hatari, lakini pia mchezaji huyo ndiye anayemfuatia Aziz Ki kwa mabao mengi, akiwa ameshafikisha mabao tisa mpaka sasa.



INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002